epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Oktoba 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581817
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**GRIEZMANN ASTAAFU UFARANSA**

UKURASA WA 2

**TRA** yavunja rekodi yake ya makusanyo tangu ianzishwe

UKURASA WA 4

**Wazee** CHADEMA waibuka na vilio kutetea kada yao nchi nzima

UKURASA WA 18

**Rwanda** yazuia mikusanyiko ya maombolezo kisa ugonjwa Marburg

BINTI WA YOMBO

# Hukumu yateka hisia za wadau

UK.2



"Ni salamu tosha kwa wahalifu kuwa uhalifu haulipi... Wakati mwingine mahakama isizuie wadau muhimu kuhusika katika usikilizaji kesi za mazingira kama haya.

**Wakili Boniface Mwabukusi**




"Hukumu hii ni ushindi mkubwa wa mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

**Mary Chatanda**



"Ninajaribu kuwaza kama wewe, kuwa hawa waliosema wametumwa, wao si ndiyo wangethibitisha huko mahakamani? Kumbuka mimi na wewe hatuna mamlaka ya kuingilia shauri la mahakamani...

**Waziri Dk. Dorothy Gwajima**



"Tunaona haki imetendeka, wito wetu ni kwamba kesi zingine ziwe zinachukua muda mfupi kama hii...

**Dk. Anna Henga**



## Wengi wafurika kuotesha vipara nywele Muhimbili

UKURASA 7



# NSSF yanuia kufikia theluthi ya watanzania

• **Yajipanga** kwa vijana kuanzia miaka 15 hadi 'mababu'...*Endelea ukurasa 3*

MICHEZO KAMATI YAWAKINGIA KIFUA WAAMUZI UK.24 KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu usimamizi wa sheria na ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TRA yaandika rekodi mpya makusanyo

**Na Grace Mwakalinga**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imevunja rekodi yake ya makusanyo, ikikusanya zaidi ya Sh. trilioni 3.1 kwa mara ya kwanza ndani ya mwezi mmoja (Septemba mwaka huu).

Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati anatoa taarifa ya utekelezaji na usimamizi wa mapato ya kipindi cha robo mwaka (Julai hadi Septemba) mwaka huu.

Alisema kiwango cha makusanyo hayo hakijawahi kufikiwa na mamlaka hiyo tangu kuasisiwa kwake.

Alisema kuwa tangu akabidhiwe majukumu ya kuongoza mamlaka hiyo, kuanzia mwezi Julai hadi Septemba mwaka huu, waliweka lengo la kukusanya kiasi cha zaidi ya Sh. trilioni 7.4, lakini wamevuka lengo kwa kupata zaidi ya Sh. trilioni 7.7.

Mwenda alisema mafanikio hayo yanatokana na usimamizi mzuri wa sheria za kodi, kuzuia mianya ya rushwa, kuweka mazingira rafiki ya ulipaji kodi pamoja na kusikiliza na kutatua vikwazo vinavyowakabili wafanyabiashara.

"Tumeandika historia mpya tangu mamlaka yetu ianze kazi. Kwa mara ya kwanza mwezi Septemba mwaka huu pekee tumefanikiwa kukusanya kodi kiasi cha zaidi ya Sh. trilioni 3.1.

"Ni jambo la kujivunia na kupongeza wafanyakazi na walipakodi wote nchini, mafanikio haya yanatokana na kusikiliza na kutatua vikwazo vya wafanyabiashara kwa wakati," alisema Mwenda.

Aliongeza kuwa mafanikio hayo yametokana na maagizo aliyoyatoa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuhusu TRA katika kutimiza majukumu yake, akihitaji uadilifu, usawa, kusimamia sera nzuri za uwekezaji na kujenga uhusiano mzuri na walipakodi ili kuhakikisha kodi stahiki inakusanywa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo.

Alifafanua kuwa TRA waliweka lengo ambapo kwa mwezi Julai walifanikiwa kukusanya asilimia 105 ya mapato, Agosti alikuwa asilimia 104 na Septemba 105.

Alisema kuwa TRA wataendelea kutekeleza maagizo ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuwasikiliza wafanyabiashara, kuwafuata walipo na kuweka mazingira sawa ya kufanya biashara kila mmoja kulipa kodi stahiki bila upendeleo.

Alisema kuwa ili kufanikisha hayo, Watanzania wanapaswa kudai na kutoa risiti wakati wa ununuzi na uuzaji.

Aliongeza kuwa TRA wamekusudia kuweka nguvu na kuimarisha kitengo cha ukaguzi na uchunguzi ili kudhibiti mianya ya upotevu mapato, yakiwamo maeneo ya forodha.

Kamishna wa Forodha, Juma Hassan, alisema wamepanga kuboresha usimamizi wa mifumo ya kuhudumia wateja wao, ambayo itaanza kutumika kuanzia Januari mwaka 2025.

Alisema mifumo hiyo itafanya kazi hata kwa mteja akiwa ofisini kwake na itaokoa muda na gharama za kufuata huduma hiyo katika ofisi za forodha, alidai mifumo itasomana.

Kamishna wa Idara ya Walipakodi Wakubwa, Michael Muhoja alisema asilimia 43 ya mapato ya TRA inatokana na kodi za wafanyabiashara wakubwa. Alisema katika kutekeleza majukumu yao wamegawana majukumu; kuna watumishi wanaohudumia masuala ya madini, viwanda na taasisi nyingine.

Kamishna wa Kodi za Ndani, Alfred Mregi aliwataka wafanyabiashara kutunza kumbukumbu zao, kutii sheria za ulipaji kodi na kuzingatia nyakati za kulipa kodi ili kuepuka faini.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
26.09.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **01.10.2024** hadi **08.10.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha Magari matupu yenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea Mlandizi kisha **Bandari ya Dar Es Salaam,** gari hizo zenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202 DSOOTG GP/NRB53910, NRB69149/NRB15200**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - Mita 36.5**
   **Upana - Mita 4.30**
   **Kimo - Mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Banadari ya Dar Es Salaam kupitia barabara ya Morogoro, Barabara ya Mandela** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# Hukumu kesi ya 'Binti wa Yombo' yawaibua wadau

**Augusta Njoji na Paul Mabeja,**

DODOMA

HUKUMU ya kifungo cha maisha gerezani katika kesi ya kubakwa na kulawitiwa binti mkazi wa Yombo Dovya, Dar es Salaam, imeibua furaha kwa wadau wa sheria na haki za binadamu.

Wamesema wamefurahishwa namna kesi hiyo iliyovuta hisia kitaifa, ilivyoendeshwa kwa haraka na kutoa hukumu wanayodai inatenda haki.

Hata hivyo, wameshauri shauri la afande anayedaiwa kuwatuma vijana hao nalo liendeshwe haraka ili kukamilisha utoaji haki dhidi ya tukio hilo.

Akizungumza jana na Nipashe kwa simu, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga alisema hukumu ya kifungo cha maisha gerezani na faini waliyopigwa na mahakama katika kesi hiyo, imetolewa kwa wakati na kwa kufuata Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, inayoelekeza adhabu ya namna hiyo kwa mtu ambaye amefanya kosa la kubaka kwa kundi.

"Tunaona haki imetendeka, wito wetu ni kwamba kesi zingine ziwe zinachukua muda mfupi kama hii, hasa za jinai, kuna kesi zinachukua muda mrefu, miezi minane hadi mwaka," alisema.

Mwongozo wa Utendaji wa Mahakama unaelekeza kesi ndogo zishughulikiwe na mahakama ndani ya kipindi kisichozidi miezi sita na kesi kubwa zisikilizwe ndani ya kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Hata hivyo, ripoti ya ukaguzi maalum wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2020/21 kuhusu haki jinai nchini, inabainisha kuwapo ukiukwaji wa mwongozo huu katika utendaji wa mahakama, hali ambayo anaitaja inasababisha kuwapo msongamano mkubwa wa mahabusu katika magereza nchini.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, Mkurugenzi Dk. Anna pia alisema wanahitaji kuona watu wote waliohusika katika tukio la Binti wa Yombo kubakwa na kulawitiwa, wanafikishwa mahakamani, akiwamo afande anayedaiwa alituma vijana hao kufanya ukatili huo.

"Kesi yake isikilizwe na haki ikamilike kutendeka," alitamka kwa hisia kali Mkurugenzi huyo wa LHRC.

**WAZIRI GWAJIMA**

Kupitia mtandao wake wa X, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, juzi alirusha taarifa ya hukumu hiyo na kuibua maoni ya wasomaji.

Mmoja wa wasomaji hao aliandika, "Tunashukuru kwa wote tuliochukizwa na lile tukio, walau mmetufuta machozi. Watanzania hii ndiyo haki tunayoililia. Sasa swali vipi kuhusu afande?"

Kutokana na swali hilo, Waziri Gwajima alisema, "Ninajaribu kuwaza kama wewe, kuwa hawa waliosema wametumwa, wao si ndiyo wangethibitisha huko mahakamani ambako mimi na wewe hatukuwapo. Kumbuka mimi na wewe hatuna mamlaka ya kuingilia shauri la mahakamani...

"Ila hao waliohukumiwa ndiyo walikuwa na fursa ya kusema tulitumwa na ushahidi huu hapa na mahakama iamue. Hivyo, ninaomba niishie hapa kuheshimu uamuzi wa mahakama tulivyosikia na ambaye hajaridhika, ninadhani huwa kuna fursa ya rufani. Asante sana," alisema Waziri Gwajima.

**MWABUKUSI**

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi alisema hukumu hiyo ni salamu tosha kwa wahalifu kuwa uhalifu haulipi.

"Nimefarijika sana kwa hukumu hii na kwa usikilizwaji wa kesi hii kwa wakati, lakini wakati mwingine mahakama isizuie wadau muhimu kuhusika katika usikilizaji kesi za mazingira kama haya," alisema Mwabukusi.

**MARY CHATANDA**

Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) pia imepongeza Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma kwa kile inachodai "kutenda haki kwenye kesi hiyo".

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Mary Chatanda alisema, "UWT inatoa pongezi kwa mahakama kwa kusimamia sheria na haki kwa kuhakikisha waliofanya kitendo hiki cha kinyama wanapata adhabu stahiki na ni ushindi mkubwa wa mapambano dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia."

Alisema UWT inatoa wito kwa watanzania kulaani vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyoendelea kukithiri katika jamii, yakiwamo matukio mawili yaliyotokea hivi karibuni mkoani Tanga, ili kulinda haki na utu wa binadamu.

Juzi Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma iliwahukumu kifungo cha maisha gerezani pamoja kulipa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja vijana wanne waliokutwa na hatia ya kumbaka na kumlawiti binti huyo.

Waliohukumiwa na Hakimu Mkazi mfawidhi wa Mahakama hiyo, Zabibu Mpangule ni aliyekuwa Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), MT 140105 Clinton Damas, maarufu Nyundo, aliyekuwa Askari Magereza C.1693 Praygod Mushi, Nickson Jackson 'Machuche' na Amin Lema, maarufu Kindamba.

## HABARI KITAIFA

# NSSF yanuia kufikia theluthi ya Watanzania



Baadhi ya wahariri ambao Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umewatambua kama watu wa mfano kwenye ustahimilivu kwa kutochukua michango yao hadi walipofika muda wa kustaafu kwa mujibu wa sheria, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wazee jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umesema unatarajia kuandikisha wanachama milioni 21 kutoka sekta isiyo rasmi, huku umri wa kuchangia ukiwa ni kuanzia miaka 15 hadi 70 na kiwango kikianzia Sh. 30,000 na zaidi kwa mwezi.

Aidha, watu walio kwenye ajira wanaruhusiwa kuchangia michango yao kama namna nyingine (uchangiaji wa hiyari) ya kuweka akiba ya uzeeni kupitia mfuko huo.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mashomba, alikuwa akizungumza na wahariri wa habari kuhusu safari ya kuelekea kutoa huduma kwa sekta isiyo rasmi kwa kuwa na skimu maalum kwa ajili hiyo.

Katika kuadhimisha Siku ya Wazee Duniani jana, NSSF ilitoa tuzo maalum kwa wahariri ambao wamekuwa wastahimilivu kwa kutochukua michango yao kwenye mfuko hadi walipotimiza kigezo cha umri kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii.

Pia ilitoa tuzo kwa waajiri wa sekta ya habari wanaopeleka michango ya wanachama wao kwa mujibu wa sheria bila kuchelewesha na ITV ilikuwa moja ya kampuni za habari zilizokidhi vigezo hivyo.

Akizungumza na wahariri, Mashomba alisema uchangiaji wa hiyari ni muhimu kwa walioajiriwa kwa kuwa unalengo la kuongeza akiba yake mtu atakapofikia umri wa kustaafu ambako mahitaji ni makubwa, na kwamba kuna wastaafu 30,000 wanaolipwa mafao ya Sh. bilioni 11.

Akiwasilisha mada ya safari ya kuelekea kutoa huduma kwa sekta isiyo rasmi, Mkurugenzi wa Uendeshaji wa NSSF, Omary Mziya, alisema sekta isiyo rasmi imeanzishwa kwa mujibu wa sheria kwa madhumuni ya kuhudumia wananchi waliojiajiri wenyewe katika shughuli za kiuchumi.

Alisema madhumuni ya kuanzisha skimu ni kuongeza wigo wa Hifadhi ya Jamii kwa makundi ambayo hayajafikiwa na huduma hizo ingawa wanashiriki kikamilifu kuchangia uchumi wa nchi, kusaidia juhudi za serikali za kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi, kuongeza nguvu za uzalishaji mali na kukuza uchumi wa nchi, na kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Mziya aliwataja wanufaika wa skimu hiyo kuwa ni mwananchi aliyejiajiri katika sekta isiyo rasmi kama kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji mdogo wa madini, sanaa mbalimbali, biashara ndogo, mama lishe/baba lishe, bodaboda, machinga na wanahabari wa kujitegemea.

Aidha, alisema mtazamo na malengo ya hifadhi ya jamii katika umri wa kufanyakazi ni kuhakikisha kila mtu anajiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kujiwekea akiba ya uzeeni.

Aidha, alisema kukosekana kwa mipango mahususi ya Hifadhi ya Jamii katika umri wa kufanyakazi kunasababisha uwezekano wa watu wengi kuingia kwenye umaskini wa kipato katika umri wa uzee.

> “NSSF imeboresha mifumo ya TEHAMA na hadi kufika Juni mwaka huu asilimia 80 ya huduma zote zitakuwa zinatolewa mtandaoni, ikiwa ni ongezeko kutoka asilimia 40 miaka mitatu iliyopita.

“Lengo la Hifadhi ya Jamii baada ya kustaafu ni kutoa kinga dhidi ya kushuka kwa kipato, kuhakikisha mstaafu anapata huduma zote muhimu ikiwamo chakula, malazi, mavazi na huduma za afya. Hali ya maisha baada ya kustaafu kutategemeana na jinsi ulivyojiandaa wakati ukiwa kwenye ajira. Maandalizi endelevu na ya uhakika ni kuwa kwenye mpango wa Hifadhi ya Jamii.

Alisema majukumu ya skimu ni kuelimisha wanachama, uandikishaji, kukusanya michango na kulipa mafao, huku vigezo vikiwa ni Mtanzania wa Tanzania Bara, mwenye umri wa miaka 15 hadi 70, asiwe ni mnufaika wa mafao ya pensheni kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini, awe na namna ya NIDA au kitambulisho chochote kinachomtambua (leseni ya udereva/ Mpigakura).

Alipoulizwa kuhusu vitambulisho na takwa la umri wa miaka 18 ndipo uvipate, alisema kwa ambao hawajatimiza umri huo watapokewa na kuunganishwa kwenye mfumo hadi watakapofikisha umri ndipo watatakiwa kuwa navyo kwa ajili ya kuwaunganisha kwenye mifumo.

“Kwa sasa vijana wadogo wanaanza kufanya kazi na kujiajiri tangu wakiwa na umri wa miaka 15, tumewawekea utaratibu kwa sababu tunajua wanakuwa hawajapata vitambulisho, ila wakishafikisha umri lazima wawe navyo kwa ajili ya kuwaunganisha kwenye mfumo,” alisema.

Kuhusu kiwango cha kuchangia, Mziya alisema kiwango cha michango ni Sh. 30,000 au zaidi kwa mwezi, na kwamba mwanachama anapaswa kutumia namba ya kumbukumbu (control number) kuwasilisha michango yake, na inaruhusiwa kuchangia kidogo kidogo kwa siku, wiki, mwezi, muhula au msimu.

Mziya alisema mwanachama anaweza kulipa michango kwenda mbele kwa muda wa miezi 12, ikiwa ameshindwa kulipia kila mwezi kutokana na chanzo cha kipato kuwa cha msimu, na kwamba akishindwa kulipa atasruhusiwa kuchangia michango kurudi nyuma kwa kipindi kisichozidi miezi 12.

Aidha, alisema michango ya kipindi kisichozidi miezi 12 kitakacholipwa hakitotozwa adhabu, huku mafao yatakayotolewa ni ya muda mrefu ya pensheni ya uzeeni, urithi, ulemavu, ya muda mfupi ni uzazi, matibabu, kujitoa (sehemu ya michango isiyozidi asilimia 50 au malipo ya mkupuo ya michango yote) na msaada wa mazishi.

Awali, Mkurugenzi Mkuu Mashomba alisema ukuaji wa sekta ya hifadhi ya jamii kwa waajiri na waajiriwa ni asilimia 70, huku msisitizo mkubwa ukiwa kwa sekta isiyo rasmi ili iweze kunufaika na huduma hiyo muhimu kwa maisha ya uzeeni.

Alisema NSSF imeboresha mifumo ya TEHAMA na hadi kufika Juni mwaka huu asilimia 80 ya huduma zote zitakuwa zinatolewa mtandaoni, ikiwa ni ongezeko kutoka asilimia 40 miaka mitatu iliyopita.

“Wanachama wetu wengi walikuwa wanalazimika kuja kwenye ofisi zetu kupata huduma, sasa tumekuja na portal inayomwezesha mwanachama kuhudumiwa popote alipo kwa kupitia simu au kompyuta. Kwa sasa unaweza kuanza na kukamilisha mchakato wa mafao yako mtandaoni,” Alisema Meneja Mifumo wa NSSF, Mathayo Mihayo na kuongeza;

“Tunataka tufikie asilimia 100 ya mambo yote kufanyika kiganjani au mtandaoni, hadithi ya mteja kusumbuliwa haitakuwapo tena, tuliona wakati mwingine unawaita wazee waje ofisi kurekebisha taarifa wakati unaweza kuwatengenezea mfumo wa kuzirekebisha kwa urahisi wakiwa kokote.”




Mashuhuda wakiangalia ajali ya gari na bodaboda, iliyotokea eneo la Kwa Msangi Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. Hakuna aliyejeruhiwa katika ajali hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# ACT - Wazalendo yalia tatizo la ajira

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha ACT Wazalendo, kimewataka Watanzania kuungana kuilazimisha serikali kutekeleza wajibu wake katika kushughulikia tatizo la ajira na kuhakikisha inaondoa mazingira kandamizi kwa watu wanaofanya biashara binafsi.

Aidha, kimewataka vijana na wazazi kutumia uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu ujao wa 2025 kukiondoa Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani kwa kuwa kimeshindwa kutatua tatizo la ajira.

Wito huo ulitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara, Isihaka Mchinjita, akiwa Mlimba, mkoani Morogoro baada ya kubaini eneo hilo na mengine kuna ongezeko kubwa la vijana wanaohitimu ngazi mbalimbali za elimu lakini wanakosa ajira licha ya taifa kutumia gharama kubwa kuwasomesha.

"Mwaka huu pekee 2024/25, fedha zinazotokana na kodi takribani Sh. bilioni 800 zitatumika kusomesha watoto wa vyuo vikuu zinatolewa kama mikopo.

"Kwa wanafunzi ni kodi zenu ambazo zinatozwa kwenye mazao nyingine mnaponunua bidhaa mnakatwa VAT (kodi ya ongezeko la thamani). Tunafanya haya kila mwaka lakini ajira zinazozalishwa kila mwaka ni chache," alisema Mchinjita.

Alisema kila mwaka vijana milioni moja wanaingia kwenye soko la ajira wakati uwezo wa serikali kuajiri kwa sasa ni vijana 70,000 tu kwa mwaka na kwamba kila mwaka vijana 930,000 wanarudi mtaani wakiwa hawana ajira. Imefikia mahali serikali haijui kesho ya kizazi cha taifa hili." Alisema.

Kuhusu watumishi, alisema sekta ya elimu kuna upungufu wa walimu 279,202 na watumishi wa afya 121,998 lakini serikali haijaweka mkazo kuhakikisha sekta hizo zinapata wahudumu na wafanyakazi, licha ya kuwapo kwa vijana waliosomeshwa kwa gharama kubwa.

**SIKU YA WAZEE**

Akizungumza katika Siku ya Wazee Dunia, Kiongozi wa Chama hicho, Dorothy Semu, aliitaka serikali kujenga mfumo wa bima ya afya kwa wote, ambao utahakikisha wazee wanapata matibabu bila kikwazo cha gharama.

Alishauri pia ibuni mpango wa pensheni kwa wazee wote, bila kujali kama walikuwa katika sekta rasmi au isiyo rasmi, na kwamba taifa lenye heshima kwa wazee wake lina maendeleo endelevu.

"Na haya yote ACT-Wazalendo, tumeahidi kuyatekeleza kupitia hifadhi ya jamii kwa wote, katika kuelekea kwenye maendeleo ya kweli, lazima tuwatambue wazee kama rasilimali yenye thamani.

"Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa wanaishi kwa heshima, faraja na usalama hivyo basi, serikali, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla, tuna jukumu la kushirikiana kuboresha maisha yao," alisema Semu.

Alisema mwaka huu ni wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Mwakani ni Mkuu na kwamba imekuwa mazoe kuiba uchaguzi ambayo ni haki ya msingi kwa raia kuchagua viongozi wanaowataka.

"Sasa niwaombe wazee wetu uchaguzi huu tunawakabidhi mikononi mwenu tuweze kuvuka na kushinda tuweze tekeleza sera ya ACT Wazalendo juu ya wazee kupata pensheni, huduma za afya bora na maisha yenye heshima.

"Ninawaomba Watanzania tuendelee kuonyesha upendo na kujali wazee, si kwa siku hii tu, bali kila siku. Taifa linalosahau wazee wake, linasahau mizizi yake," alisisitiza.

## Wazee wa CHADEMA waibuka na vilio kutetea kada yao nchi nzima

**Na Jenifer Gilla**

BARAZA la Wazee la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAZECHA), limeitaka serikali kufanyia kazi kero za wazee nchini, ikiwamo kutokulipwa pensheni zao kwa wakati hali inayosababisha waishi katika hali duni na umaskini.

Pia limetaka changamoto nyingine kuwa ni kukosa huduma ya afya bure licha ya sheria ya afya kuagiza hivyo, kukosa makazi, kukosa jukwaa la kutoa mawazo yanayogusa jamii zao, kutoshirikishwa katika mipango ya kiuchumi ya kuinua maisha yao ikiwamo mikopo na kuuawa kwa kuhusishwa na imani za kishirikina.

Akizungumza katika hafla fupi ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee jana jijini Dar es Salaam, Makamu Mwenyekiti wa BAZECHA, Susan Lyimo, alisema ni muhimu serikali kuzitambua na kuzitatua changamoto hizo ili kuweka mazingira mazuri kwa kundi hilo.

Lyimo alisema serikali inapaswa kuhakikisha wazee wote hata kama hawakuajiriwa, walipwe pensheni kama ambavyo wanalipwa wenzao wa Zanzibar ili kuwaondolea changamoto za maisha na jamii kuwatumia kama tunu ya taifa.

Aliitaka pia serikali kuhakikisha mabasi ya mwendokasi yanakuwa na sehemu maalum ya kukaa wazee kama ambavyo yametengewa nafasi kwa watu wenye ulemavu.

"Wazee wamekuwa wakinyanyaswa, hawaheshimiwi, hawapewi misaada ya kimsingi na hawana mfumo wa kuwasaidia. Matokeo yake tunaona wazee hata kwenye usafiri wa umma hasa kwenye mabasi ya mwendokasi Dar es Salaam, wanakosa vitu vya kukaa huku vijana wakiwa wamekalia viti bila kuwapisha," alisema.

Kutokana na hali ngumu ya maisha na kukosa stahiki muhimu zikiwamo huduma za afya, makazi na pensheni, alisema wazee nchini wamekuwa wakiuchukia uzee na kuukataa jambo lililozua usemi wa 'Wazee mwisho Chalinze, mjini wote baby'.

Aidha, alisema BAZECHA imetaka wazee hao kupigania muswada wa Sheria ya Wazee upelekwe bungeni ili ipitishwe kuwa sheria ili wapate haki zao za msingi kwa kuwa matukio ya unyanyasaji na udhalilishaji yanaendelea kwa kundi hilo kutokana na kukosekana kwa sheria ya kuwasimamia. Alisema tangu Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 ianzishwe, mpaka sasa haijabadilishwa na kuwa sheria ndiyo maana matukio ya unyanyasaji, udhalilishaji yanaendelea kwa sababu hakuna sheria ya kuwakingia kifua tofauti na Sera ya Watoto ambayo ilifanyiwa kazi ndani ya muda mfupi na matukio ya udhalilishaji yanadhibitiwa.

Alitoa wito kwa wazee kutoa ushauri bila kuchoka kwa watu wote hasa vijana na wenye mamalaka, kushiriki kikamilifu kwenye uchaguzi kwa kugombea nafasi, kupiga kura na kuhamasisha wengine kufanya hivyo.

**KUTOADHIMISHWA KITAIFA**

Alisema mwaka huu walipanga kufanya sherehe mkoani Mara lakini wameahirisha na kufanya kikanda kwa sababu mbalimbali ikiwamo kubadilishwa kwa tarehe ya uchaguzi wa serikali za mitaa kutoka Oktoba ilivyozoeleka hadi Novemba, mwaka huu.

Alitaja sababu ya pili ni kuahirishwa cha kwa uchaguzi ndani ya chama kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukamatwa na kuwekwa mahabusi kwa baadhi ya wagombea wa chama hicho.

"Hata wiki hii Kanda ya Pwani ilitakiwa iwe na uchaguzi lakini imeshindikana kwa sababu mwenzetu aliyekuwa mgombea wa nafasi ya uenyekiti yuko gerezani," alisema.

Mwenyekiti wa BAZECHA Taifa, Hashim Juma, aliwakumbusha wazee wa chama hicho kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili kupigania maslahi ya wananchi na kuacha alama.

Siku ya Wazee Duniani iliadhimishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) Septemba 14, 1990 ikiwa na lengo la kuelimisha jamii haki na stahili mbalimbali zinazohitajika kwa kundi hilo umuhimu wa uwepo wao katika jamii husika na kauli mbiu ya mwaka huu ni 'Kuzeeka kwa Heshima'.

# Jacob akwaa kigingi kingine cha dhamana

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Meya wa Ubungo, Boniface Jacob (42) maarufu kwa jina la 'Boni Yai' ameshindwa kupata dhamana kwa siku tatu mfululizo, kutokana na jopo la mawakili wa serikali kuwasilisha maombi mahakamani yaliyosababisha uamuzi wa pingamizi la dhamana yake kutokutolewa.

Aidha, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imetupilia mbali kiapo cha ziada kilichowasilishwa na upande wa Jamhuri kuiomba mahakama ikitumie kama ushahidi katika pingamizi la kutotolewa kwa dhamana ya mshtakiwa huyo.

Kada huyo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alipandishwa kizimbani katika mahakama hiyo Septemba 19, 2024 akituhumiwa kwa mashtaka mawili likiwamo la kuchapisha taarifa za uongo katika mtandao wa kijamii wa X.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, jopo la mawakili wa serikali lilipinga dhamana ya mshtakiwa kwa sababu ya usalama wake na wakili wake, Peter Kibatala alipinga hoja hiyo na kutaka mteja wake apewe dhamana kwa sababu ni haki yake kisheria.

Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga wa mahakama hiyo, baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 26, 2024 kwa ajili ya uamuzi wa dhamana ya mshtakiwa, lakini siku hiyo serikali iliwasilisha maombi ya kiapo cha ziada mahakamani.

Kutokana na hali hiyo, mahakama ilishindwa kutoa uamuzi na kada huyo akarudishwa rumande hadi Oktoba Mosi, 2024 kwa ajili ya uamuzi wa maombi ya kiapo cha ziada.

Hata hivyo, Hakimu Kiswaga jana alitoa uamuzi wa maombi ya kiapo cha ziada, alitupilia mbali kiapo hicho na kusema kuwa mahakama imepitia kesi nyingi na imejiridhisha pasipo shaka kuwa hakuna ubishani katika hoja zilizowasilishwa na upande wa utetezi za kudai kuwa kiapo hicho kimewekwa kwenye mfumo ikiwa muda tayari umepitia.

Pia, alisema hakukuwa na maana ya kuletwa kwa hicho kiapo cha ziada ikiwa tayari kesi imekwisha anza kusikilizwa hivyo hoja za upande wa serikali hazina mashiko kisheria na kuyaondoa maombi hayo.

Hakimu Kiswaga alitoa ahirisho la kesi hiyo hadi Oktoba 7, mwaka huu, kwa ajili ya kutolewa uamuzi juu ya mshtakiwa kupewa dhamana au kuendelea kubaki rumande. Mshtakiwa amerudishwa rumande, kutokana na ahirisho hilo inakuwa ni mara ya tatu kakosa dhamana.

Awali, upande wa Jamhuri uliomba mahakama mshtatakiwa asipewe dhamana kutokana na sababu za kiusalama kwa kuwa kiapo cha ziada kilichowasilishwa na upande huo kimejitosheleza na tayari kipo kwenye mfumo wa mahakama.

Wakili Kibatala alipinga hoja hiyo kwa kudai kuwa upande wa mashtaka wamewasilisha kiapo wakati kesi ililetwa kutolewa uamuzi wa kile kilichokuwa tayari kimekamilika.

Mahakama imefikia hatua ya kutoa uamuzi, kutokana na ubishani wa pande zote mbili kwa kuwasilisha kwa kiapo cha ziada cha kuiomba mahakama kukipokea na kutumika kama ushahidi katika suala la kutolewa dhamana.



Kingo za barabarani zikiwa zimeharibika baada ya kugongwa na magari bila ya kufanyiwa ukarabati, katika makutano ya Barabara ya Sam Nujoma na Sinza, Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# UWT yalaani BAWACHA kuchoma vitenge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUMUIYA ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi Tanzania (UWT) imelaani kitendo kilichofanywa na wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) cha kuchoma vitenge wanavyodai kupewa na Rais Samia Suluhu Hassan, huku wakitaka vyombo vya dola viliache suala hilo washughulike nalo kisiasa.

Video imesambazwa katika mitandao ya kijamii ikionesha BAWACHA Kanda ya Pwani wakichoma vitenge vinavyodaiwa walipewa Siku ya Wanawake Duniani mwaka jana kwa madai Rais hajachukua hatua dhidi ya watekaji na wauaji wa kiongozi wa CHADEMA, Ali Kibao.

Alipotafutwa na Nipashe jana, Katibu wa BAWACHA Taifa, Catherine Ruge, alithibitisha kuchomwa vitenge walivyopewa kama zawadi na Rais ambavyo havikuwa na picha ya Rais na kwamba kinachoonekana ni kipande kimoja ambacho alipewa mwanamke ambaye ni kiongozi wa ULINGO aliyekuwa amealikwa kwenye kongamano la wanawake mwaka jana.

Akizungumza jana jijini Dodoma, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda, alisema kitenge kimojawapo walichochoma kilitengenezwa na UWT Taifa ikiwa ni sare kwa ajili ya kongamano la kumpongeza Rais Samia kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kipindi cha miaka miwili, si kweli kwamba walipewa na Rais.

"Kongamano lililofanyika Machi 19, 2023 na toleo la kwanza la kitenge hicho lilitolewa tarehe Machi 13, 2023 hivyo ni uongo kusema kwamba Rais Samia ndio aliwagawia kitengo hicho kwa kuwa kwa tarehe iliyofanyika baraza lao kitenge kilikuwa hakijatengenezwa, bali wanachama wa BAWACHA walinunua kitenge hicho ikiwa ni sare kwa ajili ya kongamano la kumpongeza Rais Samia," alisema.

"Tuliwaalika na walihudhuria kwa wingi kitendo cha wana BAWACHA wengi kununua kitenge hicho na kuhudhuria kongamano letu ni kuashiria walikubaliana na ukweli kwamba Rais Samia ametekeleza mengi wa waliyoyaeleza kwenye Baraza Kuu la BAWACHA 8/3/2023. Wasiishie kuchoma vitenge, bali pia waeleze ukweli waliwezaje kufanya baraza hilo na wachome pia," alisema.

Alisema miongoni mwa hoja zao kuhusu Katiba Mpya, Rais alikubali kuendelea na mchakato na alisisitiza kuwa chama chake pia kimekubali, lakini lazima watanzania waelimishwe wajue Katiba ni nini na ni kitu gani na kinasemaje ndiyo wataweza kutoa mchango katika kutengeneza Katiba wanayoitaka kwa maendeleo ya taifa na asingependa suala la Katiba Mpya liwe takwa la wanasiasa.

"UWT pia hatuungi mkono matukio yanayotokea ya utekaji na mauaji mbalimbali nchini, tunalaani matukio hayo kwa nguvu zote. Bado tuna imani na vyombo vyetu vya usalama vinavyoendelea kuchukua hatua mbalimbali hapa nchini.

"Matukio haya yasiwe sababu ya kuvunja amani ya nchi yetu bali tuungane kama taifa kukemea na kusubiri uchunguzi wa vyombo," alisema.

Alitoa rai kwa vyombo vya dola kuhusu tukio la kuchoma vitenge waachane nalo, halina tija wala mvuto na watashughulika nalo kisiasa.

"Sisi UWT wanawake wenzao 'saizi' yetu, vyombo vya ulinzi na usalama visiwape promo, tunawaasa BAWACHA waache michezo ya kitoto, tushindane kwa hoja.

"Sisi UWT katu hatutochoma vitambara vyao maana hatuna haja ya kuwa tuliona hatuna haja ya kuwa navyo kwa vile hawana mchango wowote katika taifa hili, tunaendelea kuwaonya kuwa watulizane, hiki kibiriti kina njiti na zinawaka, ninarudi wachezee ndevu, dola haichezewi," alisema.

Alisema Rais aliwathamini, aliwaheshimu na alitambua kuwa wote ni watanzania na kukubali mwaliko wa kuwa mgeni rasmi kwenye baraza lao mwaka jana.

Alisema kitendo hicho kiliingia katika historia dunia ya kuwa na Rais kutoka chama tawala kuhudhuria mkutano wa chama cha upinzani na tuzo waliyotoa kwake alistahili kutunukiwa.

Ruge, akitoa ufafanuzi wa suala hilo, alisema, "Sisi tuligaiwa vitenge vya kawaida kama zawadi na Rais na havikuwa na nembo, ndivyo vilivyochomwa, pale kwenye video kinaonekana kitenge kimojawapo chenye picha ambacho kiongozi wa Ulingo, alipewa kwa ajili ya kongamano na hakukishona, alikuwa nacho, si kweli kwamba tulinunua, sisi hatuwezi kununua vitenge vya UWT."

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Heshima pekee kwa wazee ni kuwajali, kuwapa haki zao

**TANZANIA** jana iliungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Wazee Duniani. Maadhimisho haya hufanyika kila mwaka kutokana na Azimio Na.45/106 la Umoja wa Mataifa ambalo lilitenga Oktoba Mosi, kila mwaka kuwa siku ya Kimataifa ya Wazee na kuanza rasmi mwaka 1991.

Tangu kuanzishwa kwa siku hiyo, Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuadhimisha lengo likiwa kuhakikisha jamii inajengewa uelewa na kutiwa hamasa kuhusu kulinda haki, ustawi na maslahi ya wazee.

Mbali na lengo hilo, jamii pia, hasa wale ambao hawajafikia hatua ya uzee, hukumbushwa na kutambua kuwa uzee hauepukiki na kila anayeomba na umri mrefu anaombea kufikia uzee na hakika, anaombea afikie uzee mwema, hivyo hana budi kumpenda na kumheshimu mzee wa leo. Kwa maneno mengine, jamii inakumbushwa kuwa watoto, vijana na watu wa makamo wa leo ni vijana wa kesho, hivyo wasiwadharau, kuwanyanyasa hata kuwanyanyapaa wazee.

Kama kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka 2024 inavyosema "Tuimarishe Huduma kwa Wazee, Wazeeke kwa Heshima", kundi hilo linastahili heshima kwa kuboreshewa mifumo yao, ikiwamo upatikanaji wa huduma mbalimbali kama vile afya, malazi na makazi bora, ulinzi na usalama.

Katika kutimiza azma hiyo, kila mdau ana wajibu wa kufanya yale yanayopasa. Serikali kwa upande wake, inapaswa kuhakikisha wazee wanapatiwa matibabu kwa kutengewa dirisha maalum pamoja na bima ya afya, kuwapo kwa sera ya wazee inayoendanaa na wakati wa sasa. Pia inafahamika kwamba wazee ni kundi ambalo limetoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya taifa, hivyo linapaswa kupewa kipaumbele katika huduma mbalimbali. Aidha, kumekuwa na changamoto zinazowakabili wazee kama vile malipo ya pensheni baada ya kustaafu na pia kucheleweshwa mafao yao baada ya kustaafu kuhu baadhi ya maofisa wa mifuko ya jamii wakiwazungusha na kutengeneza mazingira ya kutaka watoe rushwa ndipo watimizie haki zao.

Jamii, kwa maana ya watu walio karibu na wazee hao pamoja na ndugu na jamaa, wanapaswa kuwalea wazee kwa misingi iliyo bora ili waendelee kuishi badala ya kuwanyanyasa hata kuwafanyia vitendo vya unyama vikiwamo mauaji kama ambavyo imekuwa ikiripotiwa katika baadhi ya maeneo.


Ni jambo la kutia moyo kwamba serikali katika taarifa yake kuelekea kwenye maadhimisho hayo, ilisema katika kuboresha mifumo mbalimbali ya maendeleo na ustawi wa wazee, iko kwenye hatua za mwisho kukamilisha kuhuisha Sera ya Wazee. Kuhuishwa kwa sera hiyo ni dhahiri kwamba ni hatua ya kuelekea kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali za kundi hili ambalo ni tunu ya taifa. Ahadi hiyo ya serikali inaleta matumaini kwa wazee kwamba matatizo na changamoto ambazo wamekuwa wakipitia hata wengine kukumbwa na maradhi yasiyo ya kuambukiza kama vile magonjwa ya moyo, kisukari na figo ambayo yanasababishwa na msongo wa mawazo kwa sababu ya kusotea mafao yao, zitapungua kiasi kikubwa.

Hali hiyo itafikia hivyo kwa kuwapo mifumo stahiki kuhusu wazee, kutawaondolea changamoto hizo ambazo pia husababisha kupoteza maisha kutokana na mambo ambayo yanaweza kutatulika. Mbali na matatizo hayo, wazee pia wamekuwa wakilalamika kutoshirikishwa kikamilifu katika mipango ya maendeleo, kukosa jukwaa la kutoa mawazo yao hasa katika jamii jambo ambalo pia huwasababishia sononа na msongo wa Mawazo kuona kwamba wamedharauliwa. Jambo hilo pia linapaswa kuangaliwa kwa upana ili wasijione wametengwa huku jamii ikitambua wazee bado ni muhimu katika kutoa ushauri wa mambo mbalimbali yanayohusu jamii hasa kutokana na uzoefu wao, ndiyo maana kukawa na msemo kwamba uzee ni dawa.

Serikali pia ifikirie kutoa nafasi za upendeleo kwa kundi la wazee katika vyombo vya uamuzi kwa kuwa na wawakilishi kama ilivyo kwa makundi ya wanawake na wenye ulemavu. Kwa kufanya hivyo watajiona wanajaliwa na kuheshimiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Mwandishi Wetu

## Muungwana Lazima Nilonge

## Vijana wamjue, kumwiga Sokoine

**MIAKA** 40 iliyopita, Aprili 12, 1984 taifa lilimpoteza Edward Moringe Sokoine, mmoja wa viongozi bora wanaoendelea kuheshimika hata leo.

Alifariki kwa ajali ya gari iliyotokea Dakawa mkoani Morogoro, akiwa safarini kutoka Dodoma kurejea Dar es Salaam, baada ya kikao cha bunge.

Miongo minne ni muda mrefu, hivyo ni wazi kuwa mamilioni ya Watanzania hasa vijana hawamfahamu Sokoine.

Sokoine ambaye angekuwa hai leo angekuwa na miaka 86, alizaliwa Agosti 1, 1938, katika kitongoji cha Kilasho kilichoko kijiji cha Emairete wilaya ya Monduli mkoani Arusha.

Ni miongoni mwa viongozi wachache wakati huo wasomi akisoma katika Sekondari ya Umbwe, iliyoko mkoani Kilimanjaro na kubwa zaidi alikuwa mpigania uhuru jasiri akijiunga na TANU, miezi kadhaa kabla ya uhuru 1961.

Kwa vijana ambao hawamjui Sokoine ambaye, kitabu kinachozungumzia maisha yake kilizinduliwa jana jijini Dar es Salaam, wafahamu kuwa alikuwa anaipenda Tanzania na mtetezi wa wanyonge.

Mathalani, anaelezwa kuwa alipoapishwa kuwa mbunge wa jimbo la Maasai, cha kwanza alipoingia bungeni anahoji hatima ya Wamasai, akiuliza haya:

"Inakuwaje Wamasai wa Ngorongoro wanakatazwa kulima, wakati hawana mifugo wala kitu cha kuwapatia chakula?"

Kadhalika anawaambia wabunge wapasue vichwa, akisema tangu uhuru yapo makabila yamefikia maendeleo makubwa lakini mengine yapo nyuma akitaka maelezo ya serikali kuwaelimisha walioko nyuma kimaendeleo ili walingane na wengine waliosonga mbele zaidi.

ALichokuwa akikitazama ni Wamasai na Watanzania wengine ambao hawakuwa na barabara, shule, maji safi, umeme na hospitali.

Kwa masuali yake hayo na mengine inaonyesha kuwa Sokoine alipenda usawa na ulinganifu kwenye maendeleo.

Alichukia umaskini tena ndani ya taifa ambalo lina rasilimali nyingi kama Tanzania. Alikuwa mzalendo ambaye tangu mwanzo alitamani maisha ya viongozi na raia yawe ya kiuadilifu na yasiyosujudu ubinafsi.

Vijana wasiomjua Sokoine wajifunze kupenda vyao na kuipenda nchi yao na nyumbani kwao pia. Hasa vijijini wanapotoka. Sokoine anaelezwa kuwa akiwa miaka 27 aligombea na kushinda ubunge jimbo la Masai na kuazimia kuleta mabadiliko.

Kwa angalizo hilo vijana nao wabadilike wasiendelee kuogopa kupiga kura na kushiriki shughuli za kisiasa hasa uchaguzi wa serikali za mitaa ulio mbele yao.

Utawasikia wakijidanganya kuwa hawawezi kupigakura maana siasa haiwahusu huko ni kukosa mwamko wa kisiasa.

Ni lazima kujituma na kushiriki mikutano ya kisiasa, vijijini kwenye vitongoji, mitaa na katika masuala yote yanayohusu maendeleo.

Pamoja na mambo mengine Sokoine anasifika kwa kuchapakazi hadi Mwalimu Nyerere na timu nzima ya TANU mwaka 1972 ikiona anafaa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akipewa majukumu makubwa kitaifa.

Mwaka 1977 anakuwa Waziri Mkuu wa Tanzania ni kutokana na utendaji kazi wake makini, ambao vijana wanatakiwa kuuiga leo. Baadhi ya vijana wa sasa hawapendi kujituma hata shuleni wanatamani watu kuwafanyia mitihani.

Wengi wanapendelea kufanyiwa kila kitu kuanzia mawazo kwa sababu idadi kubwa si wabunifu, lakini pia siyo watu wa kutafuta maarifa wala kuchangamka ili kubadili maisha yao.

Kuna mamia ya vijana wako kwenye vituo vya mabasi mfano jijini Dar es Salaam, wakiwabughudhi abiria kuwauliza iwapo wanakwenda mikoani wawapeleke kwenye mabasi ya mikoani.

Wapo wengine maelfu wanapiga debe stendi kuita abiria wanaokwenda maeneo mbalimbali wakijiita wapigadebe.

Wapigadebe wanapiga kelele vituoni wakati mabasi yameandikwa yanapokwenda, yote hayo ni kutokupenda kufanyakazi. Vijana badilikeni na kumuiga Sokoine kwa kufanyakazi na kujihusisha na shughuli rasmi zinazojenga maisha yenu, ya jamaa zenu hasa nyumbani vijijini mnapotoka.

Sokoine hakulala kwa ajili ya kubuni mbinu, kupanga mipango ya kuiletea Tanzania maendeleo, vijana wa leo mara ngapi wanakesha wakitafuta mbinu za kujiondoa kwenye umaskini na kufikia hali bora za maisha yajayo?

Ni vizuri kujitafuta na kujipata ili kuwa sehemu ya watu wanaoacha alama kwenye maisha yako na ya wengine kama alivyofanya Sokoine.

## HABARI KITAIFA




Janeth Kwilasa (wa pili kushoto), akichangia hoja wakati wa kongamano la Sahara Sparks 2024, lililowakutanisha wadau mbalimbali wa ubunifu, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uoteshaji nywele kipara wawavutia wengi Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

KITENGO cha Upasuaji Rekebishi na Upasuaji wa Urembo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kinafanya upasuaji wa aina hiyo kwa wagonjwa 12 hadi 15 kwa wiki, huku mahitaji yakiendelea kuongezeka.

Huduma zinazofanywa mara kwa mara ni pamoja na upasuaji rekebishi kwa majeruhi wa ajali za viwandani, barabarani, matukio ya moto; kukiwa na wastani wa wateja (wagonjwa) sita hadi wanane kwa siku. Hospitali hiyo ya hadhi ya juu zaidi kitaifa imesema kuwa miongoni mwa wanaohitaji huduma ya upasuaji rekebishi na idadi yao ni kubwa, ni wanaume wenye kipara.

Bingwa wa Upasuaji Rekebishi na Upasuaji Urembo MNH, Dk. Edwin Mrema, aliyasema hayo wiki iliyopita alipozungumza na Nipashe, jijini Dar es Salaam. Mwandishi wa gazeti hili alitaka kufahamu kuhusu huduma zinazotolewa katika kitengo hicho.

Alisema nchi hivi sasa ina wataalamu 10 pekee waliobobea katika upasuaji rekebishi na upasuaji wa urembo.

Alisema kitengo chao kimejikita kufanya urekebishaji wa mwonekano wa mwili, hususan wa nje kwa watu ambao wamepata ajali, wenye makovu, kasoro za mdomo, pua, masikio na kichwani.

"Kazi yetu ni kurekebisha kasoro au pale ambapo pameharibika kutokana na kasoro za duniani kama ajali au kuzaliwa. Kitengo hiki takribani miaka 18 au 20 taaluma hii inatolewa hapa ndani katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

"Huduma ambayo ni mpya ni ya kurekebisha au kufanya upandikizaji wa nywele katika kipara imeanza mwaka jana, imewavutia wengi hasa wanaume. Wengi wanaona kipara ni jambo la kawaida, ila wache hawafurahii, wanaona ni mwonekano usiowafaa kwa wakati huo.

"Tumekwishawafanyia upasuaji wanaume sita ambao wanataka kuondokana na kipara, wanaendelea vizuri.

"Upandikizaji nywele ni kama unavyootesha mpunga shambani, tunafanya kwa awamu hadi miezi mitatu au sita nywele zimeota," alisema bingwa huyo.

Alisema takwimu zinaonesha kipara hakichagui jinsi, huwakumba zaidi wazee kuanzia umri wa miaka 70 hadi 80 ingawa vijana walio katika umri wa kati ya miaka 20 huweza kuwa na hali hiyo pia.

"Kwa asilimia 33 wanaume watakuwa na kipara kuanzia miaka 30 na kuendelea na watahitaji upandikizaji nywele. Na wanaume wakifika miaka 50 kwa asilimia 50 watakuwa na uwezekano wa upungufu wa nywele.

"Wengi wao kwa asilimia 66 wakifikia miaka 60 watakuwa na upungufu wa nywele. Tukiangalia wengi wao duniani kulingana na asili, wanaoongoza kuwa vipara ni wazungu, Waasia, wakifuatwa na watu weusi (Waafrika) na kwa idadi ya chini sana ni Red Indians (Wahindi wekundu)," alisema bingwa huyo.

Dk. Edwin anataja sababu za baadhi kuwa na vipara ni pamoja na kurithi, kutokuwa na uwiano sawa wa homoni, msongo wa mawazo, lishe duni, mshtuko), homa na utapiamlo.

"Matumizi ya 'contraceptives' (uzazi wa mpango), dawa za kufifisha goita kwa watu wa kundi hili huweza kusababisha nywele kupotea. Na mwingine kuwa na kipara haina sababu na hawa siyo 'candidate' wazuri wa kuwafanyia upasuaji wa kuwapandikiza nywele," alisema.

***USIKOSE KUFUATILIA KESHO KATIKA GAZETI HILI MAKALA MAALUM KUHUSU KIPARA NA MATIBABU YAKE MUHIMBILI***

## Viongozi AMCOS wapandishwa kizimbani kwa shtaka la kughushi

**Na Mwandishi Wetu,** LIWALE

VIONGOZI wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha Twende Pamoja AMCOS wamefunguliwa kesi ya jinai na Jamhuri wakikabiliwa na shtaka la kughushi nyaraka.

Katika kesi hiyo Na. 27817 ya mwaka 2024, washtakiwa hao ni Zamoyoni Mmango, Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Twende Pamoja AMCOS na Rajab Ngaigara, Katibu wa Chama cha Msingi Twende Pamoja AMCOS.




Washtakiwa hao walipandishwa kizimbani jana katika Mahakama ya Wilaya ya Liwale mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Liwale, Christopher Makwaya.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanakabiliwa na kosa moja ambalo ni kughushi nyaraka kinyume cha vifungu vya 333, 335(a) na 337 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu [Sura16, Marejeo ya Mwaka 2019].

Ilidaiwa mahakamanin huko kuwa washtakiwa kwa tarehe tofauti kati ya tarehe 9 Machi 2022 na tarehe 11 Aprili 2022, katika kijiji cha Kitogoro, wilayani Liwale, mkoani Lindi, kwa pamoja na kwa nia ovu ya kuhadaa, walighushi nyaraka ya Sh. 10,000,000/- (milioni kumi) yenye kichwa cha habari 'Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Chama Uliofanyika tarehe 09.03.2022' kana kwamba nyaraka hiyo ni halali na imeidhinishwa kwenye kikao kwa ajili ya mkopo, jambo ambalo washtakiwa walifahamu kuwa si kweli.

Washtakiwa wote wawili walikana mashtaka dhidi yao na wako nje kwa dhamana baada ya kukamilisha masharti yaliyotolewa na mahakama.

Kesi imepangwa kutajwa tarehe 21 mwezi huu kwa ajili ya kusikiliza hoja za awali na kuanza kusikilizwa.

Kesi hii inaendeshwa na Mwendesha Mashtaka Joseph Emanuel wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Lindi.

Lindi Jumbo
Limited

JOB VACANCY

GENERAL MANAGER

**Location:** Matambarale, Ruangwa District, Tanzania.
**Closing Date:** 16 October 2024, 4:00PM (GMT+2)
**To apply and view more details visit:** https://jobportunities.net/jobs_search.aspx



**For assistance on the portal, please contact the Tara Nawa team at +264 (0) 64 402403, WhatsApp +264812294611**
**Alternatively send an email via the recruitment portal's Contact Us page.**

# Askari uhifadhi waomba nguvu kudhibiti wanyamapori waharibifu

**Na Jenifer Gilla**

ASKARI wa Uhifadhi wa Kijiji (VGS) katika Kijiji cha Likuyu Sekamaganga, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma wameiomba serikali kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi kuwasaidia vifaa vya kisasa ili kuongeza nguvu ya kudhibiti wanyamapori waharibifu.

Aidha, wamewaomba wadau hao kuwapa posho kila mwezi ili iwasaidie katika mahitaji yao ya kila siku na kuwaongeza morali ya kuendelea kufanya kazi kwa kuwa kwa sasa wanaifanya kwa kujitolea huku hali ya maisha yao ikiendelea kudhoofika.

Mmoja wa askari hao, Hassan Mkonde, aliwaambia waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kuwa vifaa wanavyoihitaji ni mabomu ya machozi yenye uwezo wa kwenda mbali, buti, sare za kazi, usafiri na mahema ya kulalia wakiwa kwenye doria.

Alisema vifaa wanavyotumia sasa kukabiliana havina nguvu ya kudhibiti makundi ya wanyama hao, akitoa mfano mabomu ya moshi kuwa hayana uwezo wa kwenda mbali na kulazimika kuyasogelea makundi ya tembo na kuhatarisha maisha yao.

"Tembo wanatabia ya kujihami, kwa hiyo akikuona unazidi kumsogelea lazima atakukimbiza ili akudhuru, tunashukuru tumepata mafunzo ya namna ya kukabiliana nao, lakini tunaweza maisha yetu hatarini," alisema.

VGS Juma Nchimbi alisema uhaba wa vyombo vya usafiri hasa pikipiki unasababisha wanachelewa kwenda kudhibiti makundi ya tembo pale wanapoletewa taarifa kwa sababu wanalazimika kutembea kwa miguu ilhali eneo la mashamba lipo mbali na kilipo kijiji.

Alisema pia wanapokuwa lindoni wanalazimika kulala kwenye maeneo ambayo si salama na kuhatarisha maisha yao kwa kuwa wanaweza kuvamiwa na wanyama au kupata magonjwa hali inayowakatisha tamaa kuendelea na kazi hiyo.

Naye VGS Juma Kibanda, alisema upatikanaji wa chakula wanapokuwa kwenye majukumu yao ni changamoto kubwa hali inayowalazimu achangishane pesa.

Aliiomba serikali iwakumbuke na kuwaweka katika mipango ya kuwapa posho za kila mwezi ili ziwasaidie kutunza familia zao na hata kumudu kujihudumia chakula wanapokuwa lindoni.

Aidha, Kibanda alilishukuru Shirika la Maendeleo ya Ujerumani (GIZ) kwa kuwapa mafunzo na mbinu za kisasa za kudhibiti wanyamapori ambazo zinawasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na wanyama hao hali iliyosaidia kupunguza uharibifu wa mazao mashambani.

Mratibu Mshauri wa GIZ Wilaya ya Namtumbo, Chrian Zimbaiya, alisema wanashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kutatua changamoto za askari hao ikiwamo upungufu wa sare za kutendea kazi na mahema.

"Ilivyoonekana kuna upungufu wa sare za kazi na sisi tuna bajeti kidogo, sasa tupo katika mchakato wa kuongeza sare 11 kwa hiyo zitaongezeka, lakini pia tunanunua mahema matatu kwa maaskari wa wilaya na baadaye tutafika na huko kwingine," alisema.

Aidha, aliwakumbusha wakazi wanaoishi kwenye maeneo yenye wanyamapori waharibifu kutumia dawa zenye harufu kali kwenye mashamba yao kutokana na asilimia 80 ya mashamba yanayovamiwa hayajawekwa dawa hizo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (kushoto), akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, baada ya kuwasili mjini Musoma jana, kuanza ziara ya kikazi ya siku nne mkoani humo. Kulia ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Gerald Kusaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watafiti wapewa jukumu chanzo ongezeko kina Ziwa Tanganyika

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika (LTA), amewataka watafiti kutoka nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika kushirikiana kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha kuongezeka kwa kina cha maji cha ziwa hilo ili kudhibiti hali hiyo inayoathiri mazingira.

Sylvain Mukanga alitoa rai hiyo jana wakati akifungua Mkutano wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Ziwa Tanganyika ngazi ya wataalamu wa kujadili kuongezeka kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika, unaofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia jana hadi leo.

Alisema mkutano huo unaowahusisha wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, wizara za kisekta na wataalamu wengine kutoka Zambia, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ulete suluhu ya changamoto ya kujaa kwa maji katika ziwa hilo.

Mukanga alisema kuwa kina cha Ziwa Tanganyika kimekuwa kikiongezeka kila mwaka kutokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu, ukiwamo ukataji miti na uvuvi haramu, hivyo ni wakati sasa wa kujadili namna bora ya kupunguza changamoto hiyo.

"Tangu mwaka 2019, mvua kubwa iliyonyesha katika kipindi hicho imesababisha mafuriko, mmomonyoko wa ardhi na upepo mkubwa na hivyo kusababisha kina cha maji cha Ziwa Tanganyika kuongezeka, hii ni hatari kwani mafuriko hayo yameleta athari katika miundombinu iliyopo katika maeneo mbalimbali yanayozunguka ziwa," alisema.

# Wakazi walia ukosefu wa maji hadi ziara ya waziri

**Na Beatrice Moses**

BAADHI ya wakazi wa Saranga, Ubungo mkoani Dar es Salaam, wamehoji maji kupatikana wakati Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alipofanya ziara, lakini sasa ni zaidi ya miezi miwili hayajatoka katika maeneo yao.

Hatua hiyo imewafanya wananchi hao kuishutumu Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuwa inafanya kazi kwa woga.

Hayo yalijiri mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye mkutano wa hadhara na wananchi huo, uliofanyika kwenye viwanja vya ~~ofisi ya serikali ya mtaa huo, ul~~ioongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hassan Bomboko, ambaye alisikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wakazi hao.

Musa Hamis, mmoja wa wakazi hao, alisema ni jambo la kushangaza kuwa mahali maji yanatiririka ovyo kutoka kwenye mabomba yaliyopasuka kiasi cha kuharibu barabara wakati kuna mahali watu hawapati maji, mafundi wakiitwa hawafiki kwa wakati.

Naye Fred Chuku alisema yeye ni miongoni mwa wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa nyumba 10 lakini DAWASA inawapa wakati mgumu hasa wakati wa kuomba kura kwa kuwa watu wanasumbuka kwa kukosa maji, hivyo hawana furaha, kwa kero hiyo inapaswa kushughulikiwa.

Diwani wa Saranga, Laiser Naigisa, baada ya kukaribishwa kuzungumza na wananchi katika mkutano huo, alisema DAWASA inawagombanisha na wananchi kwa kuwa wakati wa ziara ya Waziri maji yalikuwa yanapatikana.

"Hii inakuwa kama vile ni hujuma inayofanywa kwa wananchi ili watu wanaouza maji wafanye biashara yao hiyo," alisema.

Akijibu malalamiko ya baadhi ya wananchi, Mhandisi wa Miradi wa Mkoa wa kihuduma DAWASA Kinyerezi, Zephania Masaga, alisema changamoto ya kukosekana kwa maji katika maeneo hayo inasababishwa na mambo mbalimbali ikiwamo jiografia ya eneo hilo ambalo lina miinuko ambayo husababisha maji yakiwa na msukumo mdogo kushindwa kupanda.

Alitumia nafasi hiyo kuwasihi wananchi kuwa wepesi kutoa taarifa DAWASA pale wanapobaini kwamba kuna mabomba yanavuja maji katika maeneo yao ili mafundi wafike kwa wakati kuziba mabomba hayo na kupusha upotevu wa maji.

Wananchi walitaja maeneo kadhaa ambayo hayana maji kwa miezi miwili sasa ambayo ni Mashujaa, Kwa Mpapura na Mnarani, Majeshi.

Juni 30, mwaka huu, Waziri Aweso aliamuru Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, kukaa pembeni kwa muda na kumsimamisha kazi Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji wa DAWASA, Shaban Mkwanywe, kwa madai ya uzembe uliosababisha visima kutokuwa na maji na kuwafanya wananchi kukosa maji.

Aweso alitangaza uamuzi huo baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika ofisi za DAWASA zilizoko Ubungo akitafuta sababu za kukosekana maji mkoani Dares Salaam.



# Madaktari wa Samia wawafikia maelfu ya wagonjwa nchini

**Na Jaliwason Jasson,**

BABATI

WIZARA ya Afya imesema kampeni ya madaktari bingwa na bobezi maarufu 'Madaktari wa Samia' imewafikia wagonjwa 69,797 nchini na kuwapatia matibabu.

Juzi, Naibu Katibu Mkuu Wizara hiyo, Ismail Rumatila, alisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), walizindua mpango huo Mei 6, mwaka huu ili kuwasogezea huduma za matibabu za kibingwa na kibobezi wananchi nchini.

**Kampeni hiyo ambayo iko katika Mkoa wa Manyara kwa sasa kwa muda wa siku sita, imewahudumia wagonjwa 3,528.**

Kampeni hiyo ambayo iko katika Mkoa wa Manyara kwa sasa kwa muda wa siku sita, imewahudumia wagonjwa 3,528.

Rumatila, alisema kupitia mpango huo zimeanzishwa wodi maalumu za watoto wachanga na watoto waliozaliwa na uzito pungufu (njiti) na upasuaji wa magonjwa ya ndani.

Alisema kupitia programu hiyo, wodi za watoto wachanga na njiti 129 na hospitali 28 zilisajiliwa kuweka mpango kazi wa kuanzisha wodi za wagonjwa mahututi ndani ya miezi sita ziwe zimeanza.

Naibu Katibu Mkuu huyo, alisema kampeni hiyo mkoani Manyara imeongezewa muda wa siku moja baada ya idadi kubwa ya watu kujitokeza.

Alisema wagonjwa wa nje walikuwa 2,964, waliolazwa 311, upasuaji 150 na warufani 103.

Awali, Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga, aliipongeza wizara hiyo kwa kuratibu zoezi huku madaktari bingwa na bobezi wakizifikia halmashauri zote saba za Manyara.

Sendiga, alisema kuanzishwa kwa utaratibu wa madaktari hao kuwafuata wagonjwa mikoani kumeokoa gharama za kusafiri kwenda Dar es Salaam, Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza kufuata matibabu kwenye hospitali kubwa.



Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Muheza, mkoani Tanga, Dk. Jumaa Mhina, akizungumza na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji wakati wa semina ya mafunzo ya siku moja, juzi. Wa pili kulia ni Ofisa Uchaguzi Wilaya ya Muheza, Zaituni Abdul Said. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Serikali kujenga sekondari za amali kila mkoa

**Na Allan Isack,** MOSHI

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk.Wilson Mahera, amesema serikali imeanza kutekeleza mpango mkakati wa ujenzi wa shule za sekondari za amali kwa kila mkoa kwa ajili ya wanafunzi kujifunza kwa vitendo.

Dk. Mahera aliyasema hayo juzi katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda wakati wa kilele cha Maadhimisho ya miaka 25 ya Shule ya Sekondari ya St. Mary Goreti.

Alisema serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imewekeza katika sekta ya elimu ikiwamo miundombinu rafiki ya wanafunzi kujifunzia na walimu kufundishia.

"Ndugu zangu wananchi mliofika katika maadhimisho haya napenda kuwajulisha kuwa serikali na wizara yetu tumeweka mpango mkakati wa kujenga shule za sekondari za amali kila mkoa ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwa vitendo zaidi," alisema Dk. Mahera.

Alisema kuna uwekezaji mkubwa umefanyika kwenye sekta ya elimu, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa ya kisasa katika shule za msingi na sekondari kila mkoa nchini.

Alisema wazazi na walezi wanapaswa kuwa na moyo wa kuchangia ili kuunga jitihada za serikali.

Aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanafunzi wanapokwenda shule wanapata chakula cha mchana kwa kuwa ni wajibu wao.

"Kama mnakumbuka kuna ule Mpango wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa miaka sifuri hadi minane, hivyo ni jukumu la wazazi na walezi kuhakikisha mtoto anapata lishe bora kwa kuwa ukitaka awe na akili ni lazima umpatie chakula kizuri kwa kuwa itamsaidia kuwa na uelewa mzuri," alisisitiza.

Kwa upande mwingine, alisema serikali inatambua uwekezaji uliofanywa na Shirika la Watawa wa Bibi Yetu wa Kilimanjaro (CDNK), chini ya Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi katika nyanja mbalimbali ikiwamo ya elimu.

# Mabilioni kuboresha miundombinu LITA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI ya Poland na Tanzania, zimetenga Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini (LITA), hasa katika Ndaki ya Tengeru iliyopo mkoani Arusha.

Akizungumza jana jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe, alisema kuwa serikali inaendelea na upanuzi wa LITA katika ndaki (kampasi) zote nchini ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi soko la ajira.

"Mradi huu ni mmoja ila kuna miradi mingine midogo minne, mradi wa kwanza ulikuwa ni ujenzi wa sehemu ya kukamulia maziwa kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi walio chuoni hapo.

...Mradi wa pili ni malisho ambao utakuwa wa umwagiliaji na upo katika hatua za mwisho, muda si mrefu tutaanza uzalishaji wa uhakika na wafugaji watapata chakula cha mifugo yao na mradi wa nne ni vifaa vya maabara," alisema Profesa Shemdoe.

Alisema mradi wa tatu ni wa ujenzi wa darasa ambalo litatumika kufundisha vijana uchakataji wa maziwa.

Alisema wanaishukuru Poland kwa miradi hiyo ambayo ni matokeo ya serikali ya diplomasia ya uchumi ya kuendelea kufungua nchi katika nyanja mbalimbali.

Alifafanua kuwa kati ya fedha hizo, Poland itatoa Sh. bilioni moja na ya Tanzania Sh. milioni 500.

"Hapa tunatoa astashahada ya mifugo kwa wanafunzi wa nje na kuna kozi fupi kwa wafugaji sio wa Tengeru tu hata maeneo mengine, wafugaji watanufaika na teknolojia hiyo na faida kubwa ambayo itapatikana ni uzoefu kwa Watanzania ambao ni wengi kwenye mradi huo," alisema Profesa Shemdoe.

Awali, Mtendaji Mkuu wa LITA, Dk. Pius Mwambene, alisema serikali imetoa Sh. bilioni sita kwa ujenzi wa kumbi nne za mihadhara na ukarabati wa maabara chuoni hapo, mradi mpya wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 216 kwa wakati mmoja.

Dk. Mwambene, alisema mwaka huu serikali imetenga Sh. bilioni tatu zilizotolewa na Benki ya Dunia (WB) kukarabati miundombinu ya Ndaki ya LITA Tengeru na Morogoro.

Ushirikiano wa Serikali ya Poland na LITA Ndaki ya Tengeru, unatokana na kuwapo makaburi ya raia wa nchi hiyo walifia katika eneo hilo wakati wa vita ya pili ya dunia.



# Magereza wawaombea misaada wafungwa

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

JESHI la Magereza wilayani hapa Mkoa wa Geita limeiomba jamii kuwatembelea wafungwa gerezani na kuwapatia msaada wa mahitaji muhimu ili waweze kujikimu katika maisha yao ya kifungoni.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Mrakibu Msaidizi wa Magereza, Samwel Juma kwa niaba ya Mkuu wa Gereza la Wilaya ya Geita wakati akipokea misaada ya wafungwa iliyotolewa na vijana wa Kanisa la Habari Njema Jimbo la Geita.

**Misaada waliyotoa kwa wafungwa ni pamoja na magodoro, mafuta ya kupaka, sukari, taulo za kike, sabuni na vitenge.**

Juma, alisema gerezani kuna wafungwa wapo walio na makosa na wasio na makosa, lakini wote wanatambuliwa kisheria na kwamba wanahitaji msaada.

Alisema kipindi ambacho wanatumikia kifungo jela, ni muda wao wa kujutia yale waliyoyatenda wakiwa uraiani, hivyo jamii inapaswa kuwasaidia na si kuwatenga.

"Watu walioko gerezani wanahitaji misaada ya aina mbalimbali hivyo ni muhimu kuwakumbuka mara kwa mara ili na wao wapate mahitaji hayo muhimu," alisema.


Askofu wa kanisa hilo, Tryphone Ndikazi, alisema maandiko matakatifu kwenye Kitabu cha Mathayo 25:43-45 yanaelekeza kutenda matendo ya huruma kwa wafungwa, wagonjwa na wengine wenye mahitaji maalum kama ambavyo wao walifanya siku hiyo ikiwa ni maadhimisho ya kilele cha wiki ya vijana wa kanisa hilo.

Alisema katika maadhimisho hayo waliwatembelea wajawazito, watoto waliozaliwa kabla ya miezi tisa 'njiti' na wachanga katika hospitali ya mji Geita.

Mwenyekiti wa vijana hao, Fideli Francis, alisema kanisa hilo kila mwaka linaadhimisha wiki hiyo kwa kusaidia makundi ya jamii na kuchangia damu.

Misaada waliyotoa kwa wafungwa ni pamoja na magodoro, mafuta ya kupaka, sukari, taulo za kike, sabuni na vitenge.

Kwa wajawazito na watoto katika hospitali hiyo wametoa misaada yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 1.5.




Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Shaibu Ndemanga (wa pili kushoto), akipokea sehemu ya madawati 100 kutoka kwa Mkurugenzi wa wateja wa nje wa Benki ya Stanbic, Omary Mtiga, katika Shule ya Sekondari Kikaro iliyoko Miono, Chalinze, mkoani Pwani. Benki hiyo, pia ilikabidhi miche ya miti 100 pamoja na marekebisho ya madarasa 12 na matangi ya maji 4 yenye ujazo wa lita 5,000 kila moja, vyenye thamani ya Sh. milioni 30. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia kuhitimisha mbio za Mwenge Mwanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuhitimisha mbio za Mwenge wa uhuru kitaifa katika Uwanja wa CCM Kirumba mkoani hapa, Oktoba 14, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, maadhimisho hayo yatatanguliwa na ibada maalum ya kumbukizi ya miaka 25 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere itakayofanyika asubuhi katika Kanisa Katoliki.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana kuhusu kilele cha mbio hizo kwa miaka 60 kitaifa, Mtanda, alisema maadalizi yote yamekamilika na kwamba mwenge huo unatarajiwa kuanza kukimbizwa mkoani hapa Oktoba 6, mwaka huu.

Alisema ukiwa mkoani hapa, Mwenge huo, utatembelea na kukagua miradi 58 ya maendeleo katika halmashauri zote nane yenye thamani ya Sh.bilioni 99.3.

"Kilele hicho kitanguliwa na kumbukizi ya miaka 25 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kupitia ibada maalum itakayoongozwa na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza, Renatus Nkwande katika Kanisa la Nyakahoja kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa moja," alisema Mtanda.



Awali, alisema kutakuwa na kongamano la wiki ya vijana kitaifa kuanzia Oktoba 8 hadi 13.

Alisema kongamano hilo litafunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Oktoba 10, mwaka huu.

Mtanda, alisema katika kongamano hilo kutakuwa na maonesho ya kazi mbalimbali za vijana.

"Kutakuwa na mabanda zaidi ya 120 ambako vijana kutoka maeneo mbalimbali nchini watapata fursa ya kuonesha shughuli zao," alisema.

Alisema kwa vijana waliopata mikopo ya asilimia kumi kutoka halmashauri nchini, watapata fursa ya kujadili mchango wao katika ujenzi wa taifa.

Katika hatua nyingine; Mtanda amesema ofisi yake imeandaa mbio maalum Oktoba 12, mwaka huu kwa lengo la kuhamasisha wananchi kushiriki katika kelele mbio hizo za Mwenye wa uhuru.

Alisema washindi katika mbio hizo watapata zawadi fedha.

## Askofu ahimiza amani uchaguzi

**Na Samson Chacha,** TARIME

ASKOFU wa Kanisa Katoliki Jimbo la Musoma, Michael Msoganzila amewahimiza wananchi kudumisha amani iliyoko nchini katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na mkuu mwakani.

Askofu Msonganzila alitoa kauli hiyo juzi wakati wa harambee ya ujenzi wa kanisa hilo iliyofanyika Parokia ya Nyamwaga iliyoendeshwa na mchapishaji maarufu wa vitabu nchini, Nyambari Nyangwine.

Alisema kanisa hilo litaendelea kuhubiri amani hasa katika kipindi cha chaguzi hizo ili kila Mtanzania aendelee kuidumisha na kuitunza ili isiharibike.

Askofu huyo alionya kuwa endapo Amani na utilivu havitalindwa, hakuna atakayetamani kuendelea kuishi nchini kama ilivyo kwa mataifa mengine.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo kuwa na upendo kwa kila mmoja bila kujali itikadi zao za siasa.

Askofu huyo alimshukuru Nyangwine ambaye aliwahi kuwa mbunge wa Tarime Vijijini kwa kufanikisha harambee hiyo iliyosaidia kupatikana zaidi ya Sh. milioni 200, zikiwamo zaidi ya Sh.milioni 42 alizochangia.

Akizungumza wakati wa harambee hiyo Nyangwine, aliwaomba waumini wa kanisa hilo kuhakikisha wanashiriki kuchangia miradi ya maendeleo ya afya, maji, elimu na dini badala ya kuiachia jukumu hilo serikali.

Katika hatua nyingine; Nyangwine ametoa msaada wa vitabu vyenye thamani ya Sh.milioni tisa kwa Shule ya Kisangura ili kusaidia wanafunzi katika masomo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Meja Edward Gowele, ambaye pia alishiriki katika harambee hiyo, aliwaomba waumini hao kujitokeza katika chaguzi hizo ili kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo.

Gowele, vilevile aliwataka wafanyabiashara na watu wenye uwezo wa kifedha kuchangia maendeleo kwa jamii ili kuiunga mkono serikali kuwaondelea kero wananchi.




Ukurasa 13

**Viongozi watoto waanza kushirikishwa kuukabili ukatili wa kijinsia mtaani**



Ukurasa 14



**MIAKA 40 BILA SOKOINE Watanzania kwa kubadili fikra ndiko kumuenzi zaidi Sokoine**



# Wanamapinduzi Kusini mwa Afrika, China kumuenzi Nyerere

• Ni wiki ijayo mdahalo kuziibua, kuchambua uhalisia fikra zake

**Na Lugenzi KABALE, MJNL Kibaha**

OKTOBA 14 kila mwaka Tanzania na wapenda amani na maendeleo duniani hufanya kumbukizi ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Ndiye aliyeiongoza nchi kwa mafanikio kati ya mwaka 1961 hadi 1985 alipong'atuka uongozini, ameiachia Tanzania amani na mshikamano.

Nyerere ni kiongozi wa pili kustaafu kwa hiari madaraka ya urais barani Afrika, akifuata nyayo za Rais wa kwanza wa Senegal, Leopold Sedar Senghor aliyestaafu 1980 na kumkabidhi madaraka aliyekuwa Waziri Mkuu wake, Mamadou Dia Abdou Diouf.

Ni kwa msingi huo waliokuwa wapigania uhuru wa Afrika Kusini, Zimbabwe, Angola, Msumbiji, Namibia na CCM Ijumaa ijayo Oktoba 11 wanakutana Kibaha kwa Mfipa mkoa wa Pwani kumuenzi Mwalimu Nyerere.

Ni katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere -Julius Nyerere Leadership School (MJNLS) kwenye mdahalo wa kuukumbuka na kuenzi mchango wa Baba wa Taifa katika harakati za ukombozi Afrika.

Profesa Marcelina Chijoriga, Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere anaeleza kuwa mdahalo huo unatarajiwa kuhudhuriwa na wageni 200 kutoka ndani na nje ya nchi.

Anafafanua kuwa utaendeshwa kwa kauli mbiu "Mwalimu Nyerere na Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika: Tafakuri ya Mshikamano, Uongozi, Umajumui na Umoja wa Afrika".

Aidha, Profesa Marcelina, anasema utafunguliwa rasmi na



Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Professa Marcelina Chijoriga, kada wa CCM Steven Wasira, Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara mstaafu, Phillip Mangula. **PICHA: MWANDISHI WETU**

rais mstaafu Jakaya Kikwete.

Anaongeza kuwa rais mstaafu amethibitisha kufungua na kushirika mdahalo huo ambao pia unatarajiwa kuhudhuriwa na Thabo Mbeki rais mstaafu wa Afrika Kusini na Mkuu wa Majeshi wa Zimbabwe, Luteni Jenerali, Anselem Sanyatwe.

Taarifa zaidi za mdahalo huo zinaonyesha kuwa mada tisa zitawasilishwa na kujadiliwa zikiwa na maudhui mbalimbali kuhusu Mwalimu Nyerere na harakati za mapambano ya ukombozi wa Afrika.

Mada hizo pamoja na watakaoziwakilisha katika mabano ni Uongozi na Urithi: Matokeo ya Maono ya Mwalimu Nyerere kwa Viongozi wa Sasa wa Afrika(Thabo Mbeki), na Jukumu la Mwalimu Nyerere katika Mapambano ya Ukombozi Afrika, Kanali mstaafu wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), Joseph Simbakalia.

Mada zaidi zitakazowakilishwa na kujadiliwa ni ile inayotolewa na Mkuu wa Majeshi ya Zimbabwe, Luteni Kanali, Sanyatwe atakayezungumzia "Changamoto na Fursa za Kuendeleza Dira ya Nyerere: Mtazamo kutoka kwa vyama Rafiki Sita".

Kwa upande wake Mwakilishi wa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) atajikita katika andiko lenye mada "Ujenzi wa Msaada wa Nyerere katika Uhusiano wa Kimataifa na Afrika.

Dk. Charles Mubita Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama tawala Namibia SWAPO, atazungumzia "Jukumu la Elimu ya Itikadi katika Kuhifadhi Alama ya Nyerere."

Itakumbukwa kuwa vyama vya CCM, MPLA cha Angola, ZANU PF ya Zimbabwe, ANC ya Afrika Kusini, FRELIMO cha Msumbiji, SWAPO ya Namibia, na Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) kwa pamoja vinamiliki chuo cha MJNLS.

Vyama hivyo vitawakilishwa na Stephen Wasira MNEC na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM.

"Komredi Wasira atawasilisha mada ya Maono ya Mwalimu Nyerere kuhusu Afrika kujitegemea kiuchumi huku mjumbe wa Bodi ya Usimamizi ya MNJLS inayoundwa na wawakilishi kutoka CCM, SWAPO, MPLA, FRELIMO, ANC, ZANU PF na CPC, Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda akitoa neno la shukurani na kufunga mdahalo huo," anafafanua Profesa Marcelina.

Historia ya harakati za ukombozi inasema kuwa mara baada ya kupinduliwa kwa serikali ya Rais, Kwame Mkrumah wa Ghana 1966, Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika ililazimika kuhamishia makao makuu Tanzania, baada ya serikali kukubali kuipokea.

Kuwapo kwa makao makuu ya Kamati ya Ukombozi ya OAU kulifanya vyama vya kupigania uhuru vya Guinea Bissau na Cape Verde, ZANU PF, ZAPU PF vyote vya Zimbabwe na ANC, PAC na SACP vya Afrika Kusini kuhamishia makao yake Dar es Salaam.

Au kuwa na ofisi za uwakilishi hapa nchini hali iliifanya Tanzania kuwa kinara wa harakati za mapambano ya ukombozi wa Afrika.


Vyama vya ukombozi wa ANC na PAC, ZANU-PF chini ya uongozi wa Dk. Robert Mugabe, SWAPO kikiongozwa na Sam Nujoma, FRELIMO ikiiongozwa na Erduado Mondlane na baadaye Samora Machele vilikuwa na makambi ya kufundishia wapigania uhuru wa majeshi ya ukombozi ya vyama hivyo.

Makambi ya wapigania uhuru hao yalikuwa katika mikoa ya Iringa (Mgagao), Dodoma (Kongwa), Mtwara katika Wilaya ya Nachingwea, eneo maarufu kama Farm 17, Tabora (Kigwa) na pia mkoani Morogoro (Dakawa).

"Ni Makambi ya ANC chini ya uongozi wa Oliver Tambo am-

INAENDELEA UK. 12

# Ujasusi teknolojia ya kielektroniki ulivyomwangamiza mkuu wa Hezbollah



Hassan Nasrallah, aliyeuawa na Jeshi la Israel. **PICHA: REUTERS**

**Na Mwandishi Wetu**

KIKUNDI cha Hezbollah cha Lebanon kimeumia kwa mambo mengi wiki iliyopita ikiwa ni pamoja na kumpoteza kiongozi wake Hassan Nasrallah.

Hasara nyingine imetokana na kuharibiwa vifaa vyake vya mawasiliano na simu za upepo zinazotumiwa na Hezbollah.

Kwa miaka 32 iliyopita, Hezbollah haijamjua kiongozi na katibu mkuu isipokuwa Hassan Nasrallah, ambaye aliuawa Ijumaa iliyopita katika mashambulizi ya Israel yaliyolenga makao makuu ya chama hicho kusini mwa mji mkuu wa Lebanon Beirut.

Israel ilifanya mashambulizi ya anga katika mji mkuu wa Lebanon Beirut Ijumaa iliyopita na kumuua Nasrallah.

Kabla ya hapo kulikuwa na milipuko kadhaa mwezi uliopita ulijeruhi zaidi ya wapiganaji 1,500, huku wengine kadhaa wakipoteza maisha.

Swali linaloulizwa ni kwa namna gani vikosi vya usalama vya Israel vilimsaka Nasrallah na kufanikiwa kuwalenga makamanda wakuu wa Hezbollah?

Kwa mujibu wa mwandishi wa usalama wa BBC, Frank Gardner, kumlenga Nasrallah ulikuwa uamuzi wa kimkakati wa Israel.

Anasema kwa miaka kadhaa iliyopita walikuwa wakiishi mafichoni na Israel ilikuwa ikiwafuatilia.

“Maelfu ya vifaa vya mawasiliano vya Hezbollah na simu za upepo vililipuliwa hivi karibuni. Inaaminika kuwa shirika la kijasusi la Israel linahusika.”

“Kutokana na kila kitu kilichotokea tangu wakati huo, ni wazi kuwa Israel imejikita sana katika muundo wa Hezbollah.” Anasema.

Anaongeza kuwa wakati jeshi la Israel linasema limewaondoa makamanda wakuu wote wa Hezbollah, swali ni jinsi lilivyovizuia kwa ufanisi vyombo vya usalama vya Hezbollah.

**KUPATIKANA NASRALLAH**

Kwa mujibu wa ripoti maalum ya shirika la habari la Reuters, Nasrallah alizungumza na vyanzo kadhaa vya Lebanon, Iran na Syria kabla ya kifo chake.

Shirika la habari la Reuters, likinukuu chanzo, kimoja linadai kuwa Israel ilikuwa ikifanya ujasusi dhidi ya Nasrallah na Hezbollah kwa miaka 20 kabla ya kushambulia makao yao makuu.

Maofisa wawili wa Israel wanaiambia Reuters kwamba Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu na kamati maalumu ya mawaziri waliidhinisha shambulio hilo Jumatano iliyopita.

Ni wakati huo huo, Netanyahu alikuwa akihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mjini New York, Marekani.

Matthew Saville ni Mkurugenzi wa Huduma za Kijeshi katika Taasisi ya Royal United Services, anayesema inaonekana kuwa mpango huo umekuwa ukifanya kazi kwa miaka mingi na unaweza kuwa umetekelezwa katika viwango kadhaa.

“Inaonekana kulikuwa na utekaji nyara wa mawasiliano, pia kusikiliza maagizo ya siri au mazungumzo au kupata habari kuhusu wahusika.

Aidha, huenda pia kulikuwa na ‘uchambuzi wa picha’ za satelaiti au picha zilizopigwa kwa siri ambayo ni pamoja na kupata taarifa za siri zinazotolewa na wanadamu.

Kwa maneno mengine, wapelelezi walio chini wanaweza kuwa na jukumu kubwa pia la kufuatilia na kusaka habari hizo.

Baada ya vita vya 2006 kati ya Israel na Hezbollah, Nasrallah aliacha kusafiri hadharani tena asiyeonekana kwa wepesi.

Chanzo kilicho karibu na usalama wa Nasrallah kinaliambia shirika la Reuters kwamba kiongozi huyo yuko katika hali ya tahadhari.

Anaelezwa kuweka vikwazo vikubwa na alikuwa akikutana na watu wachache sana.

Maofisa watatu waandamizi wa jeshi la Israel wanaliambia gazeti la Marekani la ‘The New York Times’ Jumamosi iliyopita kwamba walikuwa na taarifa kuhusu mahali alipo Hassan Nasrallah kwa miezi kadhaa.

Kwa mujibu wa ripoti za Israel, uamuzi wa kumlenga Nasrallah ulifanywa mara moja na bila ya kuifahamisha Marekani, ili wasipoteze muda.

Kwa mujibu wa ripoti ya Reuters, Nasrallah alikuwa katika hali ya tahadhari baada ya milipuko ya vifaa vya mawasiliano, kwani haikuwa siri kuwa Israel ilitaka kumuua.

Hakujumuishwa hata katika msafara wa mazishi ya makamanda wa Hezbollah, na hotuba zake zilizorekodiwa kabla kusikilizwa siku chache baadaye.

Israel inasema makao makuu ya Hezbollah yalikuwa chini ya jengo la makazi ya watu kusini mwa Beirut, ambapo bomu lilimlenga Nasrallah.

Jeshi la Israel linasema kuwa limewaua makamanda tisa wa jeshi la Hezbollah akiwamo Nasrallah katika muda wa wiki moja.

Magnus Ranstort wa Chuo Kikuu cha Ulinzi cha Uswizi ni mtaalam anayefuatilia masuala ya Hezbollah.

Anasema maendeleo haya ni kikwazo kikubwa kwa Hezbollah, ambayo inafichua kushindwa kwa intelijensia yake.

Magnus anasema:”Wao- Waisraeli walijua kwamba Nasrallah alikuwa akifanya mikutano, akikutana na makamanda wengine aliposhambuliwa.”

Akizungumza na waandishi wa habari Jumamosi, msemaji wa jeshi la Israel Luteni Kanali Nadav Sheshani, anasema kuwa alikuwa na taarifa za ‘muda halisi’ kuhusu mkutano kati ya Nasrallah na viongozi wengine.

Hata hivyo, Seshani hakufafanua jinsi taarifa hizo zilivyokuwa zikipatikana akisema wanakwenda kukutana ili kushambulia Israel.

Brigedia Jenerali Amichai Levin, Kamanda wa Jeshi la Anga la Hatjerim la Israel, anawaambia waandishi wa habari kwamba makumi ya mabomu yalirushwa ndani ya sekunde.

“Hii ilikuwa operesheni ngumu sana na ilikuwa imepangwa kwa muda mrefu,” anasema.

Kwa mujibu wa Saville, ndege za kivita za Jeshi la Anga la Israel F-15 zimeripotiwa kudondosha mabomu takribani 80, yenye uwezo wa kuharibu ngome hiyo, baada ya kupata taarifa halisi kuhusu eneo la Nasrallah.”

Taarifa zinasema mabomu yalirushwa yakilenga vyumba vya chini ya ardhi huko Beirut Kusini na Dahiya. Hapa ndipo Nasrallah alipokuwa akikutana na makamanda wengine.

Na kwamba kutokana na hayo yote ni wazi kwamba mashirika ya kijasusi ya Israel yalifanikiwa kupenya vyombo vya usalama vya Hezbollah.

Nafasi ya Nasrallah hivi karibuni itachukuliwa na mtu mwenye sifa zinazofanana na hizo za kidini. Lakini itamchukua miaka kiongozi huyo mpya kupata wafuasi.

## WANAMAPINDUZI KUSINI MWA AFRIKA, CHINA KUMUENZI NYERERE

**INATOKA UK. 11**

baye alikuwa na makao makuu yake huko Lusaka na ya FRELIMO ndiyo yalikuwa makubwa sana hapa nchi ambapo ANC walikuwa na kambi ya Solomon Mahlangu, Mazimbu nje kidogo ya Manispaa ya Morogoro,” anasema ofisa mmoja jina tunalo.

Akiwa mmoja wa maofisa katika Kamati ya Ukombozi wa Afrika iliyokuwa na makao makuu Dar es Salaam, anaomba jina lake lisitajwe akisema ni kinyume cha kiapo na maadili ya kazi yake.

Anaongeza kuwa katika kambi au shule ya uongozi ya ANC ya Solomon Mahlangu Mazimbu au Solomon Mahlangu Freedom College (SOMAFCO) kulikuwa na maelfu ya wapiganaji wa ANC wakipata mafunzo ya aina mbalimbali.

Anasema walifunzwa uongozi na kujitayarisha kuchukua nafasi za uongozi mara serikali ya kidemokrasia chini ya ANC itakapotwaa madaraka huko Afrika Kusini jambo lililokuja kutokea mwaka 1994 pale Nelson Mandela alipoapishwa kuwa rais wa kwanza Mwafrika.

“Kwa upande wa FRELIMO na ZANUPF pia zilikuwa na idadi kubwa ya wapiganaji wakipata mafunzo huko Kongwa, Mtwara, Mbeya, Iringa na Bagamoyo katika mkoa wa Pwani.” Anasema.

Anaongea kuwa ni katika kambi ya Bagamoyo ambapo Rais wa sasa wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, aliishi na kupata mafunzo, baadaye kuwa moja ya maofisa wa tawi la kijeshi la ZANUPF.

# Viongozi watoto waanza kushirikishwa kuukabili ukatili wa kijinsia mtaani

NA SABATO KASIKA

UKATILI wa kijinsia dhidi ya watoto, wasichana na wanawake, ni miongoni mwa matukio yanayoleta fedheha katika familia na taifa pia.

Watoto wananajisiwa, kuteswa, kupata vipigo kupindukia, kutakanwa na kunyimwa mahitaji muhimu. Na wakati wote wanaowafanyia hayo wanawaambia usimwambie mtu, ukisema nitakumaliza.

Katika juhudi za kukabiliana na ukatili kama huo, wadau wa kutetea haki za wanawake na watoto wameunda kamati za uongozi zinazoongozwa na kusimamiwa na watoto kukabiliana na migogoro na ukatili dhidi yao.

Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam kinachojihusisha na vita dhidi ya ukatili wa kijinsia ukiwamo ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni na rushwa ya ngono kimeunda kamati hizo za kiuongozi ili watoto washiriki kupiga vita.

Mwenyekiti wa kituo hicho Fatma Twalib, anaiambia Nipashe kwenye mahojiano hivi karibuni kuwa, wameunda kamati za uongozi wa watoto mtaani baada ya kubaini kuwapo kwa ukatili unaofanywa na jamaa wa karibu na wazazi kuanzia baba, mjomba, shangazi na ndugu wengine ndani ya familia lakini unafichwa.

"Tunaamini watoto hao watashirikishana kusikiliza na kufuatilia ukatili unaowakabili, kuamua migogoro yao midogo midogo na kupeleka kwenye uongozi mambo mazito," anasema.

Anaeleza kuwa iwapo watu wazima wana utaratibu na uongozi wao, hata watoto wanahitaji kuwa nao, hivyo wameamua kuwaandaa na kuuanzisha.

Anaeleza kuwa kupitia uongozi wa watoto, anaamini kuwa watakuwa wamepanua wigo kwa watoto hao kuripoti matukio ya ukatili ambayo yamekuwa wakitokea kwenye jamii.

"Tuliamua kuwakusanya katika maeneo yao wanayochezea ya kuwapa wazo hilo, wakubali na tukawapa nafasi ya kuchagua uongozi wao, wakachaguana, hivyo sasa wana uongozi wao," anasema.

Mwenyekiti huyo anafafanua kuwa, katika harakati ambazo kituo hicho kimekuwa kikifanya, wamebaini kuwa kuna mambo ambayo mtoto hawezi kumwambia mama au baba, bali rafiki yake wa karibu.

"Lakini hata rafiki yake akiambiwa, hajui ataitatuwaje changamoto hiyo, lakini kupitia uongozi tulioutengeneza, mtoto akiwa na tatizo atapeleka kwa kiongozi wao, naye atatuletea sisi, tumewapa mafunzo ya jinsi ya kutatua migogoro midogo," anasema.

Katika utatuzi huo wa migogoro midogo, Fatma anasema watoto hao wataanza kwa kesi ndogo ndogo zikiwamo za kuibiana kalamu, kutoleana matusi na kupigana.

Anasema wakifanikiwa kutatua migogoro hiyo midogo, ni wazi huo utakuwa ni mwendelezo wa mafanikio ya kufikia lengo la kituo hicho la kushirikisha watoto kutoa taarifa za matukio ya vitendo vya ukatili na ndani ya jamii vinavyoumiza watoto, wasichana na wanawake.

"Kituo cha Sauti ya Jamii tumekuja na ubunifu huu, tunatamani kuona ukiigwa nchi nzima, kwa sababu vitendo vya ukatili vimeenea kote, si hapa kwetu tu," anasema.

Anaeleza ni lazima kuchukua hatua za kuwalinda na kuwaepusha waathirika hao na ukatili lakini pia na kuwadhibiti watuhumiwa.

Anasema kwa sasa kituo kimeona ni lazima kila mmoja ashiriki kuanzia watoto ndiyo maana kituo hicho kimekuja na mbinu mpya ya kuwahusisha watoto katika vita hiyo, kwa kuunda uongozi wa watoto mtaani ili waweze kueleza katika uongozi wao madhila wanayokumbana nayo.

Anafafanua kuwa wameunda kamati tatu za ukatili, elimu na mazingira na kwamba wanafunzi uongozi wao, wamo wa darasa la pili hadi hadi la sita.

"Bado tunaendelea kupanga ratiba yao ya jinsi ya kututana kila mwishoni mwa wiki na kuweka yao ya kupambana na ukatili ndani ya familia na ndani ya jamii.



Watoto wakiwa katika uchaguzi wa viongozi wa kamati za kuwasikiliza mitaani. **PICHA: SABATO KASIKA**

> "Tuliamua kuwakusanya katika maeneo yao wanayochezea ya kuwapa wazo hilo, wakubali na tukawapa nafasi ya kuchagua uongozi wao, wakachaguana, hivyo sasa wana uongozi wao," anasema.

**SAUTI ZA WATOTO**

Mwenyekiti wa uongozi wa watoto hao Yasinta Mpoze, anasema anaamini nafasi aliyoipata ni mwanzo mzuri kwake wa kujiandaa kuwa kiongozi wa baadaye, kwa kuwa anapata uzoefu kupitia jukumu hilo.

"Walichokifanya Kituo cha Sauti ya Jamii, ni jambo jema kwetu watoto, kwani mbali na majukumu mengine tulionayo, ni kama kutuandaa kuwa viongozi wa baadaye kupitia uzoefu na mafunzo tunavyopitia," anasema Yasinta.

Anasema watoto wana mambo mengi wanayokumbana nayo yakiwamo ya kuonewa na wenzao ambao ni wababe, huku wakiogopa kuwataja na kwamba kupitia uongozi huo watawaelekeza jinsi ya kuwa huru.

Yasinta anasema yapo mafunzo ya uongozi wanayopata kituoni ambayo watayatumia kusaidia wenzao kubadili tabia na wengine na kuachana na mienendo ya uhalifu na uchokozi.

"Lakini pia tutasaidiana na kuelekezana kuacha au kuficha ukatili, badala yake watuambie ili na sisi tuyafikishe katika kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni kwa hatua zaidi," anasema.

Katibu wa uongozi wa watoto hao Stan Mhagama, anakishukuru kituo hicho kwa kuwashirikisha katika mambo makubwa ambayo jamii na AZAKI nyingi hazijafikiria umuhimu wa kutumia watoto kutatua migogoro ya namna hiyo.

Mhagama anasema yeye na viongozi wenzake watajitahidi kufanya kile ambacho wataweza ili kusaidia katika vita dhidi ya ukatili wa watoto kwa kuwa karibu na viongozi wa kituo hicho kupata uzoefu.

"Tutaongoza watoto wenzetu kadri inavyowezekana ili kusaidia watoto wenzetu kufunguka wanapofanyiwa ukatili na wazazi wao, ndugu zzao au watoto wenzao ama wanafunzi wenzao," anasema Mhagama.

Mmoja wa wazazi wa watoto hao, Oresta Mhagama anasema ushirikishwaji wa watoto unaotakiwa katika kipindi hiki ambacho dunia imeharibika na kusababisha kuwapo kwa matukio ya kutisha.

"Kuna ripoti mtoto ameharibiwa kwa kulawitiwa au kufanyia kitendo chochote cha ukatili, hasemi, lakini kupitia uongozi wao, tunaamini wale wote waliokumbana na madhila hayo wanaweza kufikisha taarifa kwa wenzao ili wayafikishe katika kituo hicho," anasema Oresta.

Oresta anaongeza: "Kuanzisha uongozi wa watoto ni hatua mojawapo ya ushirikishaji wa watoto katika vita dhidi ya ukatili ambao umeleta madhara na vifo kwa baadhi yao katika maeneo mbalimbali."

MIAKA 40 BILA SOKOINE

# Watanzania kwa kubadili fikra ndiko kumuenzi zaidi Sokoine

**Na Gaudensia Mngumi**

IMETIMIA miaka 40 tangu kifo cha Waziri Mkuu wa zamani Edward Sokoine, ambaye anakumbukwa kwa uongozi wa kuwajali na kuwatetea maskini kwa kuwapatia bidhaa na huduma muhimu kwa unafuu.

Katika kuenzi kazi zake zilizotukuka, kitabu cha 'Edward Moringe Sokoine: Maisha na Uongozi Wake', kinazinduliwa wiki hii Dar es Salaam na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kinaelezea changamoto, kazi ngumu na kujitolea kwake na mengi aliyoyafanya Sokoine wakati wa uhai wake.

Ni miaka 40 tangu kutwaliwa kwa kiongozi huyo aliyekuwa na fikra za kimapinduzi, kujitegemea na aliyewapenda sana Watanzania.

Fikra tunduizi za Sokoine zilijengeka kwenye kuwa na Tanzania inayojitegemea na kujisimamia kiuchumi na kimaendeleo na yenye usawa ili kila mmoja afanyekazi, apate huduma na bidhaa muhimu kama tiba, elimu, chakula, usafiri na ajira kwa unafuu na uhakika.

Leo mambo yamebadilika Tanzania ya Sokoine siyo ya zama hizi za mwaka 2024 Watanzania wameungwa na mataifa mengine kwenye mnyororo mmoja wa maendeleo ya sayansi na teknolojia ya kielektroniki.

Kwa mtaji huo wa kutaka kuwa na Tanzania ya kisasa aliyoitamani waziri mkuu huyo, taifa limuenzi kwa kubadili fikra na kuanza kujitambua ili kujiletea maendeleo kama alivyotaka Sokoine.

Mosi ni kwa kufanyakazi kwa bidii. Sokoine alisimamia Sheria ya Nguvu Kazi, akitaka kila mmoja afanyekazi. Leo vijana wa mijini na vijijini hawafanyikazi, wanapenda maisha na pesa zinazopatikana kwa njia rahisi.

Wanapenda kula bila kazi mfano, mijini wanakaa vijiweni wakisogoa habari za Simba na Yanga na ikifika muda wa mlo wanakimbilia nyumbani kula bila kutafuta chakula licha ya kuwa na zaidi ya miaka 20.

Wapo vijana wanaoishi kwa kubwia dawa za kulevya, kuvuta bangi na kujikita kwenye michezo ya kubeti. Pamoja nao wapo wanaojitoa kuishi kwenye 'ndoa batili' na watu wazima ili wawape chakula na mahitaji yote muhimu wakijiita mariyoo.

Katika kumuenzi Sokoine vijana wahamasishwe na wahamasike kufanyakazi kwa kutumia mikakati mingi. Ikibidi ifanyiwe mapitio mara ili kuboreshwa ilenge kubadili maisha yao na kujiondolea umaskini na uhohehahe.

KIUCHUMI

Watanzania wabadilike kwani wanaendelea na fikra kuwa sekta binafsi inawanyonya. Ni wakati wa kuiamini kuwa ndiyo nguzo ya uwekezaji na kuendeleza uchumi.



Edward Moronge Sokoine enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, zipo fikra kuwa kuwapo wawekezaji wageni mfano kwenye madini, viwanda na utalii hakujawa na tija kubwa badala yake wageni hao wananufaika zaidi kuliko wazawa.

Ipo haja ya kuachana na fikra hizo na kuamini kuwa pamoja na kuwapo kwa sekta binafsi ya wazawa na wageni ndani ya nchi, uwekezaji wa vitega uchumi vikubwa vya kigeni au 'Direct Foreign Investiments' (DFIs) ni muhimu mno kwa taifa leo.

Watanzania wakumbuke kuwa DFIs ni lazima kwa sababu ndicho kimekuwa kichocheo cha kukua uchumi kwa kasi kwenye mataifa kama China, Korea Kusini, Indonesia, Malaysia, Thailand na Vietnam ambayo miaka ya 1961 yalikuwa maskini kama Tanzania.

Kuwa na uwekezaji mkubwa wa kigeni ndiko kunakofanikisha nchi inayoendelea kama Tanzania kuvutia wawekezaji, wanaojenga viwanda, kuchakata bidhaa, kuziongezea thamani, kuajiri watu na kuziuza ndani na nje tena zikiwa na lebo 'made in Tanzania' na kupaisha kodi na mapato.

Watanzania wasiwaone wawekezaji kuwa ni wanyonyaji wafahamu kuwa DFI zina athari ya kimaendeleo katika masoko na vitega uchumi ambavyo wawekezaji watarajiwa tena wakubwa zaidi wanaweza kutumia fursa yao kufika na kuwekeza.

Kwa mfano taarifa kutoka mtandao wa China 's Econimic Raise: History, Trends...' zinaeleza kuwa mapato kutokana na uwekezaji wa FDI mwaka 2018 yalifikia Dola za Marekani bilioni 39 na kuifanya kuwa mpokeaji wa namba mbili wa vitega uchumi vikubwa kutoka nje.

Taifa la kwanza lenye vitega uchumi vikubwa vya kigeni duniani ni Marekani. Uchumi wa China umekua haraka kutokana na uwekezaji wa vitega uchumi vya FDIs.

Tanzania nayo inahitaji sana wawekezaji hao, hivyo watu wabadili fikra, hilo ni muhimu na wawathamini ili kufikia uchumi wa kimaendeleo hasa viwanda vinavyoongeza thamani na kuuza bidhaa zenye viwango za 'made in Tanzania'.

**TUSIGUSE RASILIMALI**

Watanzania wana hofu kuwa rasilimali za taifa kama madini zimelindwa kwa miaka mingi hivyo ziendelee kuhifadhiwa ardhini mpaka taifa litakapokuwa na uwezo wa kuzihudumia.

Uwezo unaomaanishwa ni wataalamu na viwanda. Ukweli ni kwamba hizo ni fikra za kizalendo lakini kwenye uchumi wa kiutandawazi suala la kuhifadhi rasilimali linaweza lisiisaidie nchi.

Kwa mfano dunia ya leo inakataza matumizi ya visukuku au 'fossil' kama mafuta, gesi na makaa ya mawe ili kulinda mazingira kwa maelezo kuwa nishati hizo zinaongeza joto mno na kutishia hatima ya dunia.

Tanzania kwa miongo mingi imehifadhi makaa ya mawe kwenye mgodi wa Ngaka uliopo Mbinga mkoani Ruvuma. Leo kuna kampuni ya TANCOAL kwenye mgodi wa Ngaka ambayo inachimba madini hayo, lakini ikumbukwe kuwa dunia inabadilika ukisema ujifungie wengine wanasonga na umuhimu wa rasilimali unayoitunza unaondoka.

Madini ya makaa ya mawe yakiendelea kuhifadhiwa yanaweza yasiwe na tija hivyo ni vyema kutumia rasilimali zilizopo kwa maendeleo.

Cha msingi ni kuwa na mikataba inayonufaisha taifa na mwekezaji wa kigeni lakini pia kuhakikisha kuwa mnyororo mzima wa kuongeza thamani unafanywa kwenye viwanda vya Tanzania na hilo ndilo la kusimamia sasa kwenye mijadala na mazungumzo na wawekezaji.

Mabadiliko ya fikra, kuacha rushwa na kuchapakazi zaidi kiuzalendo kuwe chachu ya kumuenzi Sokoine.





# Sangu ataka ushirikiano E-GA, sekta binafsi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA) imetakiwa kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuongeza wigo wa ajira kwa vijana wabunifu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini.

Wito huo ulitolewa juzi na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu wakati akifunga programu ya awamu ya tano ya mafunzo kwa vitendo na mafunzo kazini kwa mwaka huu wa fedha wa 2024/25, inayoendeshwa na e-GA kupitia Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-GovRIDC) jijini hapa.

"Naipongeza e-GA kwa kazi nzuri mnayofanya ya kukuza vipaji na kuongeza uwezo kwa vijana katika matumizi ya TEHAMA, pia nawashauri kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kutoa fursa kwa wanafunzi wanaoshiriki mafunzo kwa vitendo na mafunzo kazini katika kituo hiki kupata fursa za ajira," alisema Sangu.

Alisema ushirikiano kati ya e-GA na sekta binafsi utaongeza tija kukuza, kuimarisha tasnia ya TEHAMA na wigo wa ajira kwa vijana.

"Nimetembelea miradi inayoendelea katika kituo hiki na nimeona kazi kubwa ambayo e-GA mnaifanya ya kuwaandaa vijana wetu waweze kuendana na mabadiliko ya teknolojia mpya zinazoibukia kama vile akili mnemba na sarafu ya kidijitali na nimeona jinsi vijana wetu walivyo na uwezo mkubwa katika maeneo hayo," alisema.

Sangu aliipongeza e-GA kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha vijana wanajifunza teknolojia mpya zinazoibuka duniani kufanya bunifu za TEHAMA na kutengeneza mifumo ya kielektroniki itakayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi serikalini na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kuijengea uwezo mamlaka hiyo ili kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanazidi kuimarika na kuandaa vijana mahiri ili washiriki katika ujenzi wa Tanzania ya Kidijitali.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba, aliahidi kuendeleza na kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi na kuwajengea uwezo vijana katika TEHAMA ili kutoa fursa ya kuonesha uwezo wao katika teknolojia hiyo na kukabiliana na ushindani katika soko la ajira duniani.

"e-GA itaendeleza ushirikiano na sekta binafsi na vyuo vikuu kuwajengea uwezo vijana katika eneo la TEHAMA, kuwawezesha kushindana katika soko la ajira duniani, kufanya hivyo tutakuwa tumesaidia kupunguza changamoto ya ajira nchini," alisema Ndomba.

# Uzalishaji zao la pamba waporomoka Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amesema serikali itahamasisha wakulima mkoani hapa kutilia mkazo kilimo cha pamba ili kurejea uzalishaji hadi kufikia zaidi ya kilo milioni sita kwa mwaka baada ya kuporomoka.

Dendego aliyasema hayo juzi katika kiwanda cha kuchambua pamba cha kampuni ya Biosustain Tanzania Ltd kilichoko Manispaa ya Singida.

Ni baada ya kuelezwa kuwa kiwango cha uzalishaji wa pamba mkoani hapa kimeshuka kutoka kilo milioni sita hadi kufika kilo milioni 2.5.

**Changamoto iliyopo katika kilimo ni baadhi ya wakulima kuongeza mchanga, mawe na maji kwenye pamba ili kuongeza uzito.**

"Hatukubali kuona uzalishaji wa pamba unashuka kwa kiwango hiki, lazima tukaweke mpango mkakati wa wakulima wetu ili uzalishaji uweze kuongezeka na kufikia zaidi ya kilo milioni 6," alisema Dendego.

Alisema serikali itatoa ushirikiano katika mpango unaofanywa na kampuni hiyo wa kutaka kujenga kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula yanayotokana na mbegu za pamba.

Alisema Singida unategemewa katika uzalishaji wa mafuta ya kula ya alizeti, hivyo kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula yanayotokana na mbegu za pamba utasaidia kuongeza upatikanaji wa bidhaa hiyo nchini.

"Sisi Singida tumejipambanua kuhakikisha hili goli la dhahabu ambalo tumepewa kuweka vikwazo kwa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi kuingia nchini kwa kuongeza tozo hii ni fursa kwetu ya kuhakikisha tunazalisha mafuta kwa wingi," alisema.

Aliipongeza kampuni hiyo kwa kuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi wanawake kwa kuwa unaakisi agenda ya kufikia asilimia 50 kwa 50 kati yao na wanaume.

Mratibu wa shughuli za kilimo wa kampuni hiyo, Bether Bryton, alimweleza mkuu huyo wa mkoa kuwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka huu ni kuzalisha ajira za kudumu 139 na kufikia 410.

Bryton, alisema kampuni ina wakulima 24,000 wenye uwezo wa kuzalisha pamba mbegu kilo milioni 44 na kuzalisha pamba nyuzi kilo milioni 18 kwa mwaka.

Alisema changamoto iliyopo katika kilimo ni baadhi ya wakulima kuongeza mchanga, mawe na maji kwenye pamba ili kuongeza uzito.

Alisema changamoto hiyo inasababisha kuharibu ubora wa mbegu na pamba na soko lake la ndani na nje ya nchi kutokana na uchafu.



Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, Dk. Pius Chanya, akizungumza katika mkutano wa hadhara Kijiji cha Kilimatinde, Kata ya Solya, mkoani Singida jana. Aliwataka wananchi kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, pamoja na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Diwani awapa somo wazazi, walezi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZAZI na walezi mkoani hapa wamehimizwa kushirikiana na walimu kufuatilia maendeleo ya watoto ili wafanye vizuri kitaaluma na kutimiza ndoto zao.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Diwani wa Kata ya Ipagala ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Ngombo Dotto, wakati akizungumza na wazazi na walezi kwenye mahafali ya 15 ya Shule ya Sekondari Makole.

Dotto, alisema jukumu hilo la kufuatilia maendeleo elimu halipo kwa upande mmoja bali lipo kwa wazazi, walezi, walimu, serikali na wadau wa maendeleo wa elimu.

"Wazazi na walezi wana mchango mkubwa kuhakikisha watoto wao wana maendeleo mazuri ya kitaaluma naomba tushirikiane kwa hili, "alisema.

Akizungumza kuhusu maadili kwa wahitimu hao kidato cha nne, aliwataka kuwa na malezi bora yatakayowawezesha kuendelea zaidi kielimu na kufikia ndoto zao.

Awali Mkuu wa shule hiyo, Beatrice Mangole, alisema shule yao inakabiliwa na changamoto ya waendesha bodaboda kupita kwenye eneo hilo kwa fujo na kusababisha wanafunzi kukosa utulivu.

Aliomba serikali na wadau wa maendeleo ya elimu kuwasaidia kujenga uzio ili kuondokana na kero za bodaboda.



HABARI MBEYA

# Watoto waliokuwa wakitumikishwa mashamba tumbaku wakombolewa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya watoto 20,000 waliokuwa wameajiriwa kwenye mashamba ya tumbaku maeneo mbalimbali nchini wameondolewa kwenye ajira hiyo na kuendelezwa kielimu, huku baadhi yao wakiwezeshwa kujiajiri kwenye shughuli zingine wanazozimudu.

Watoto hao wameondolewa kutoka katika halmashauri tano zinazozalisha zao hilo ambazo ni Chunya, Songwe, Kaliua, pamoja na Mpanda.

Meneja wa Mradi wa Prosper Resert, Fred Malaso, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa kikao cha tathmini ya utumikishwaji wa watoto kwenye mashamba ya tumbaku nchini.

**mradi huo unaofadhiliwa na SLT Foundation kutoka Uswis ambalo linajihusisha na kutokomeza utumikishwaji wa watoto kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji.**

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na SLT Foundation kutoka Uswis ambalo linajihusisha na kutokomeza utumikishwaji wa watoto kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji.

"Mwaka huu pekee wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Utumikishwaji wa Watoto, tuliwasaidia baadhi ya watoto hao vifaa vya kufanyia kazi kwenye ajira zao binafsi ambazo hazina madhara kwao," alisema Malaso.

Alisema wamekuwa wakifanya kazi kwa kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine wa kutetea haki za binadamu zikiwamo za ndani na nje ya nchi.

Akifungua kikao hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogoro, aliiasa jamii kuwekeza katika kupambana na umaskini sambamba na kuwaelimisha watoto kuhusu haki zao.

Vilevile, aliitaka jamii kutumia mbinu zote kukomesha utumikishwaji wa watoto kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji, huku akiwataka wamiliki wa mashamba kuacha kuajiri watoto kwenye shughuli hizo za uzalishaji.

Alisema utafiti nyingi zinaonyesha kuwa watoto wengi wanaajiriwa kwenye shughuli za uzalishaji kutokana na hali ya umaskini kwenye familia zao.

"Tuwekeze sana kwenye kufuta umaskini, kuwaelimisha watoto kuhusu haki zao za msingi na naamini kwamba tukishirikiana kwa ukaribu tutakomesha tatizo hili la utumikishaji wa watoto," alisema Mpogoro.

Wakizungumzia hatua zinazochukuliwa na serikali katika kupambana na utumikishwaji wa watoto, maofisa kazi na ustawi wa jamii wa halmashauri zinazozalisha tumbaku waliwashukuru wadau kwa kushirikiana nao kwenye vita hiyo.

Ofisa Kazi wa Mkoa wa Songwe, Pendo Lugendo, alisema wamekuwa wakipita kwenye maeneo mbalimbali ya kazi na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu namna ya kuepuka kuajiri watoto na badala yake wawapatie kazi nyepesi za kuwafundisha.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Kaliua mkoani Tabora, Bonface Sambaya, alisema katika eneo analotoka watoto wengi wamekuwa wakitumikishwa kwenye mashamba ya tumbaku na wengine kwenye kazi za nyumbani.

Alisema mradi huo (Prosper reset) umekuja kuongeza juhudi za mapambano ambayo tayari yalishaanzishwa na serikali na hivyo akawataka wadau wengine kuunga mkono juhudi hizo.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Salim Abri Asas, akizungumza wakati akifunga mafunzo ya uongozi kwa viongozi 370 wa UVCCM kata zote za mkoa wa Iringa katika Chuo cha Vijana Ihemi, juzi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Bil.273/- kununua magari, boti, helikopta za jeshi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imewekeza Dola za Marekani milioni 100 (Sh. bilioni 273.18) kwa ajili ya kununua magari 150, boti 20, magari ya kubebea wagonjwa na helikopta za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa lengo la kuliwezesha jeshi hilo kupambana na majanga mbalimbali.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alisema hayo mkoani Njombe alipotembelea ujenzi wa ofisi na Kituo cha Jeshi la Zimamoto Mkoa wa Njombe kinachojengwa kwa Sh. milioni 700.

Masauni alisema hatua hiyo itasaidia kuondoa tatizo la vitendea kazi kwa askari na hivyo kuwa historia katika kiwango ambacho hakijawahi kutokea.

Alisema Mkoa wa Njombe utaletewa helikopta ili kudhibiti moto kwenye misitu ya miti ya kupandwa na ile ya asili, hivyo itasaidia kulinda rasilimali za wananchi.

"Ni jambo ambalo kwanza linahitaji kuwa na askari wa kutosha wa kuweza kuvitumia vifaa hivyo lakini kuwa na askari ambao wanaweledi," alisema Masauni.

Hivyo, aliwataka askari hao kutengeneza utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya kinga na tahadhari ya moto ili waweze kuwa sehemu ya kusaidia jitihada za kudhibiti majanga.

"Elimu inasaidia kufanya watu wazuie vyanzo vinavyochangia katika kusababisha madhara ya majanga mbalimbali ikiwamo moto lakini hata yanapotokea basi wananchi waweze kutoa ushirikiano kwa askari wetu," alisema Masauni.

Naye Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Njombe, Mrakibu Msaidizi Joel Mwakanyasa, alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wametengewa bajeti ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa kituo katika Wilaya ya Njombe Sh. milioni 700.

"Hadi kufikia Septemba 29, mwaka huu mradi umetekelezwa kwa wastani wa asilimia 74.2 kwa kazi mbalimbali zilizofanyika na zinazoendelea kufanyika," alisema Mwakanyasa.

Mwakanyasa alisema jeshi hilo linaendelea na kuweka jitihada za kuhakikisha inapunguza matukio ya moto kwa kutoa elimu kwa wananchi.

Baadhi ya askari wa jeshi hilo Mkoa wa Njombe akiwamo Evaristo Mng'ong'o aliomba serikali kusaidia kupatikana kwa helikopta ya kuzimia moto kwa sababu mkoa huo umezungukwa na miti.

## Dk. Tulia ahamasisha mamalishe kutumia nishati safi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewahamasisha mamalishe na wananchi mkoani Mbeya kutumia nishati safi ya kupikia hasa gesi ili kutunza mazingira na kuokoa muda wa shughuli za kiuchumi.

Pia amewasisitiza kuacha kutumia kuni na mkaa wakati wa kupikia kwa sababu inahatarisha usalama wa afya zao.

Alitoa wito huo juzi mkoani hapa akiwa na wadau wa nishati safi ya kupikia kutoka Kampuni ya Gesi ya Oryx baada ya kuwatembelea mamalishe wa Mtaa wa Uyole na kushiriki kupika chakula kwenye moja ya migahawa iliyopo katika eneo hilo.

Katika ziara hiyo alitumia gesi kupika kama sehemu ya kutoa mfano kwa wananchi kuhusu faida ya matumizi ya nishati hiyo ambayo alisema inasaidia kutunza mazingira na kuokoa muda kutokana na kupika kwa muda mfupi.

Kwa upande wake Meneja wa miradi ya nishati safi ya kupikia kutoka Kampuni ya Gesi ya Oryx, Peter Ndomba alisema wamekuwa wakisaidia makundi mbalimbali yakiwamo ya mama na baba lishe kupata nishati safi ya kupikia.





## Magonjwa yasiyoambukiza tishio Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MSAIDIZI wa Meneja Kitengo cha Maradhi Yasioambukiza kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Zuhura Salehe Amour amesema magonjwa yasioambukiza bado ni tishio Zanzibar kwa kuathiri na kupoteza viungo vya watu jambo ambalo linachangia kupoteza nguvu kazi wa taifa.

Alisema hayo wakati akifungua mkutano wa wanaharakati na watetezi wa maradhi hayo.

Alisema kutokana na ongezeko kubwa la maradhi hayo iko haja ya jamii kufuata elimu inayotolewa kwa njia mbalimbali ili kuthibiti ongezeko na vichocheo vya maradhi hayo.

Zuhura alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameanzisha mpango maalum kuhakikisha anazishughulikia saratani za aina tatu ambazo zinawapa matatizo zaidi kwa kinamama na kinababa.

Alizitaja saratani hizo ni matiti, shingo ya kizazi na tenzi dume, akisema kwa kufanyika zoezi maalum la uchunguzi wa maradhi hayo katika wilaya mbalimbali kushirikiana na wataalamu kutoka Hospitali ya Ocean Road na wanapatiwa tiba mgando.

Aidha alisema wizara imejipanga kufikia malengo kwa kutoa elimu kwa jamii kwa kushirikiana na jumuiya zisizo za serikali pamoja na mashirika mbalimbali ili kuthibiti maradhi hayo.

## Bil. 33/- kukabili athari mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya Sh. bilioni 33 zimetengwa kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika wilaya tano zilizopo katika Ukanda wa Pwani.

Wilaya hizo zitafikiwa na Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko Tabianchi II, unaotekelezwa na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji (UNCDF).

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mratibu wa Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kutoka UNCDF, Aine Mushi alisema lengo kuu ni kuwasaidia Watanzania, serikali kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Awamu ya kwanza ya mradi tulianza wilaya za Kondoa, Kongwa, Mpwapwa na Chamwino mkoani Dodoma, lakini awamu ya pili itahusisha wilaya tano za mikoa ya mwambao wa Pwani. Hivyo serikali itaainisha tuanze na wilaya zipi," alisema Aine.

Alisema wataangalia athari na namna wananchi walivyoathirika, kwamba watawezesha kufanya kilimo kitakachowaondoa katika matatizo ya mabadiliko tabianchi, pamoja na kuwa na miundombinu rafiki.

# Serikali yaeleza sababu kuanzisha bima ya wasafiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema kuanzishwa na kutekelezwa kwa bima ya wasafiri kumetokana na changamoto mbalimbali ambazo Serikali ya Zanzibar ikikumbana nazo.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Juma Makungu katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mtabwe, Dk. Mohammed Ali Suleiman, aliyetaka kujua, Je, serikali imefanya utafiti na kujiridhisha kwamba mpango wa kutoza bima hiyo hautaathiri sekta ya utalii Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Waziri Juma alisema changamoto hizo, zimesababisha serikali, kuja na hatua ya kuanzisha bima ya wasafiri ili kuwa na njia endelevu ya kuzitatua pindi zinapotokea.

Juma alisema katika kukuza utalii wa Zanzibar, serikali imeendelea kutafuta njia nyingi za kuhakikisha kuwa utalii wa Zanzibar unakuwa wa kiwango cha juu.

Alisema baadhi ya changamoto zilizokuwapo ni pamoja na Zanzibar kutokuwa na mfumo mahususi wa kuwakinga na majanga wageni wanapofika Zanzibar.

Kadhalika, alisema kutokuwa na mfumo uliokuwa unaunganishwa na bima za kimataifa, kwamba huduma hiyo mpya kwa Zanzibar siyo ngeni duniani na baadhi ya nchi zimekuwa zikitekeleza ikiwamo Qatar, Mauritius, Ulaya na Amerika.

Aidha, alisema utaratibu wa utekelezaji wa bima hiyo ulitangazwa katika Bajeti ya Serikali kupitia hotuba ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na utekelezaji wa hatua hiyo ni wa serikali kupitia Shirika la Bima la Zanzibar, chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Alisema hakuna wizara yoyote ambayo imeingiza bajeti kwa ajili ya hatua hiyo, kwa kuwa gharama zake za utekelezaji zipo katika Shirika la Bima la Zanzibar na usimamizi wake kisera upo katika Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na hauna gharama za ziada.

Alisema wakati wa janga la ugonjwa huo wageni walilazimika kutumia fedha za ziada kwa ajili ya kupata makazi ya kujitenga kwa kipindi kisichopungua siku saba, matibabu na gharama za kubaki hospitalini pindi akipata maradhi hayo na hatimaye kupelekea wageni wengi kutosafiri kwa muda kuhofia gharama hizo za ziada.

Alisema vilevile, sera hiyo ya serikali imeanzishwa na kusimamiwa na Shirika la Bima la Zanzibar pekee ni kwa sababu Zanzibar kuwa sehemu salama na yenye kuvutia wageni wengi.



Watendaji wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura Kisiwani Pemba, wakila kiapo cha kutunza siri na kujitoa uanachama wa chama cha siasa kabla ya kuanza kwa mafunzo yao ya siku mbili jana. Uboreshaji wa daftari Zanzibar utafanyika kwa siku saba kuanzia Oktoba 7 hadi 13, mwaka huu, na vituo vitafunguliwa saa 02:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni. **PICHA: INEC**

# Wizara yaeleza sababu kuingilia upandaji bei bidhaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imesema serikali hulazimika kuingilia kupanda kwa bei za bidhaa Zanzibar pale ambapo kunakuwa na upandaji wa bei holela za bidhaa zinazoingizwa nchini ikiwamo zinazotoka nchi za nje.

Waziri wa Wizara hiyo, Omar Said Shabani alisema hayo juzi katika Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakar Hamad Bakar, aliyetaka kujua ni wakati gani serikali hulazimika kuingilia kupanda kwa bei za bidhaa Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Omar alisema jambo hilo linatokana na sababu tofauti zikiwamo za upungufu wa baadhi ya bidhaa katika masoko ya nje, kupanda kwa gharama za usafirishaji, kuwepo na upungufu wa upatikanaji wa fedha za kigeni.

Alisema fedha hiyo ndiyo inayotumika kuagizia mizigo kutoka nje ya nchi, kuendelea kuwapo kwa vita duniani na uzuiaji wa usafirishaji wa baadhi ya bidhaa katika nchi zinazozalishwa bidhaa hizo.

Aidha, alisema serikali kupitia Wizara ya Biashara na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara hufanya mapitio ya bei elekezi za bidhaa kwa zile zinazodhibitiwa pale inapohitajika kufanya hivyo.

Alisema kupitia Kifungu cha 5(1), (C) cha Sheria Namba 5 ya Mwaka 2018 ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji kinatoa mamlaka ya kupanga na kusimamia bei elekezi kwa bidhaa zinazodhibitiwa na serikali kila panapokuwa na mfumko wa bei usiokua na sababu kwenye soko.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Othman Shabani, alisema ubora wa mwani unaozalishwa nchini katika uhitaji wa soko la kimataifa hadi sasa ni mzuri.

Alisema wakulima na wafanyabiashara wa mwani wanashajiishwa kuzingatia usafi wa mwani kwa kuanika maeneo salama, ili kuepuka kuwa na michanga na takataka nyingine ili kuepuka kuathiri ubora wa mwani huo.

Aliyataja maeneo ambayo ni vinara kwa kuzalisha mwani kwa wingi na kwa kiwango kinachokubalika ni Tumbe, Fundo, Shumba mjini, Chokocho, Makunduchi na Muungoni.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu maadhimisho ya kitaifa ya kuzimwa kwa Mwenge wa Uhuru yatakayoambatana na kumbukizi ya miaka 25 ya kifo cha Mwl. Julius K. Nyerere yakiongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Oktoba 14, 2024. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Taasisi zahimizwa matumizi Akili Mnemba

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wa taasisi nchini wamehimizwa kutumia teknolojia mpya, ikiwamo Akili Mnemba (AI) kuboresha utendaji wao enzi hizi za kidijitali.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Dk. Jabiri Bakari, alisema hayo wakati akiwasilisha mada kuhusu matumizi ya AI katika mkutano ulioandaliwa na Jumuiya ya Wakurugenzi nchini uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Akiwasilisha mada alisema taasisi zisiogope AI bali ziitumie kutokana na uwezo wake wa kuleta mabadiliko.

Dk. Bakari alisema AI sio kitu kipya imetokana na maendeleo ya teknolojia ya kompyuta.

Aidha, alisema AI ni nadharia ya kuandaa na kutumia mifumo ya kompyuta inayoweza kufanya kazi zinazohitaji akili na binadamu bila kutegemea binadamu moja kwa moja.

"Inahusisha mpangilio na mantiki ya kimahesabu ya hali ya juu kuwezesha kuwapo hali ambapo mifumo inaanza kufanya kazi kama binadamu," alisema.

Alisema hii ni hatua ya juu zaidi ya mifumo ya kompyuta na programu wezeshi.

"Ikumbukwe kwamba vyote hivi vinatengenezwa kwa kutegemea akili ya binadamu, na inabidi viandaliwe kufanya kazi kama binadamu," alisema.

Dk. Bakari alisema kuwa teknolojia inabadilika. Teknolojia ya sasa ya habari na mawasiliano itakuwapo na kupita, kama ilivyokuwa kwa enzi za matumizi ya zana wa mawe, chuma na ujio wa viwanda.

Alisisitiza kwamba mabadiliko ya teknolojia ni mtambuka. Mipango kwenye kilimo, miundombinu ya usafiri, uchimbaji madini, elimu na afya kwa mfano inabidi kutekeleza viwango vya utayari wa kutumia mifumo ya kidijiti, alifafanua.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU), Dk. Bakari alisemam, kuongeza matumizi ya teknolojia kwa asilimia 10 kwenye sekta mbalimbali kunaongeza ukuaji wa uchumi kwa asilimia 2.5.

Aliwajulisha washiriki kuhusu mpango wa TCRA wa kuhamasisha masomo yanayowezesha ustadi na umahiri wa kumudu teknolojia za kidijiti.

Masomo hayo ni Sayansi, Teknolojia, Uhandishi na Hisabati.

"TCRA pia inahimiza uanzishaji wa vilabu vya kidijiti katika ngazi zote za elimu kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu. Lengo ni kuwezesha uelewa wa masomo wezeshi kidjiti kutoka ngazi ya chini, jambo ambalo litafanikisha kuenea masomo yanayowezesha mifumo ya kidijiti ngazi zote," alisema.

TCRA ilifadhili washiriki watano wa Tanzania kwenye mashindano ya Hisabati kwa wanafunzi wa shule za sekondari Afrika yaliyofanyika Afrika Kusini Agosti 2024.

Aidha, watatu kati yao walishinda jumla ya medali nne za shaba, na walioshinda ni Ambrose George Rutashobya wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga; Zakaria Mataiga Mwita wa Azania na Stella Ludan Maliti wa Sekondari ya Wasichana ya Marian ambaye alipata medali mbili. Vilevile alitangazwa kuwa "Malkia wa Hisabati".

# Rwanda yatoa angalizo kasi kusambaa virusi Marburg

**KIGALI, Rwanda**

WIZARA ya Afya nchini Rwanda, imetoa mwongozo mpya kuzuia kuenea kwa virusi vya Marburg nchini humo.

Imesema, idadi ya watu waliofariki kutokana na ugonjwa huo, imeongezeka na kufikia wanane.

Dalili kuu za homa hiyo ni pamoja na maumivu makali ya kichwa, misuli, kutapika na kuhara.

Raia wametakiwa kufika kwenye vituo vya afya, pindi wakionesha dalili hizo.

Katika taarifa ya wizara hiyo, iliyotolewa juzi jioni, watu 26 waliripotiwa kuambukizwa virusi hivyo tangu Septemba 27, mwaka huu.

Huo ni mlipuko wa kwanza wa Marburg uliothibitishwa nchini humo.

Waziri wa Afya, Sabin Nsanzimana, alisema wanawafuatilia zaidi ya watu 300 ambao wanadaiwa waligusana na wagonjwa waliofariki na waliothibitishwa kuambukizwa.

Baadhi ya miongozo iliyotolewa ni pamoja na kusimamishwa kwa muda kuwatembelea wagonjwa hospitalini, kudumisha usafi binafsi na kuepuka kugusana na watu wanaoonesha dalili, ingawa shughuli za biashara zinaendelea kama kawaida.

Aidha shughuli za mazishi na maombolezo ya nyumbani pia zimepigwa marufuku, wafiwa wakitakiwa kuepuka msongamano inayoweza kuongeza hatari ya kueneza virusi hivyo, pia ufunuaji wa jeneza hautaruhisiwa katika nyumba, makanisa na misikiti.

***RFI***

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**GHARIB SAID KHALFAN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T168DLE** aina ya **Toyota RAV 4,** Chassis No. **JT172SC1100175472,** Engine No. **Z135GL.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/DOD/40546/2024**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Nelly Henry Harson,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo chenye namba za usajili **irdp/crp/14/3258** kilichotolewa na chuo cha Mipango Mwaka 2014. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/ARU/ARU/36962/2024**

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**PAULO BATON SHITINDI** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE446586** iliyotolewa na makao makuu **DAR ES SALAAM PCO.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/203943/2024**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**WOLFGANG RAMADHANI GUMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T449BAQ** aina ya Mitsubish PAJERO , Chassis No. NJ01063, Rangi ya Silver. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/DOD/41822/2024**

**TANGAZO LA NOTISI WADAIWA**

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Thelathini (30) kwa mdaiwa, Ndugu **MASHELLA SYLIVESTER KENEMO,** wa Dar Es Salaam.

**MASHELLA SYLIVESTER KENEMO** ulikopa na kushindwa kulipa deni la mkopo wako, hivyo unatakiwa kulipa deni lako la mkopo unaodaiwa na Tujijenge ndani ya siku thelathini (siku30).

Hii ni baada ya mkopo kushindwa kulipwa kulingana na masharti na makubaliano ya mkataba dhidi yako na Tujijenge.

Notisi hii ya siku thelathini (30) itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo kama utashindwa kulipa deni la mkopo ndani ya muda ulioainishwa (siku thelathini).

Ikiwa ni pamoja na kuruhusu dalali kuendelea na taratibu za kisheria za kuuza mali zako zilizotumika kudhamini mkopo uliochukuliwa.

**Kwa Mawasiliano piga:**
**+255222774742-3/0715100985/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

# Waliofariki kwenye mafuriko, maporomoko Nepal wafikia 200

**KATHMANDU, Nepal**

IDADI ya watu waliofariki nchini Nepal kutokana na mafuriko na maporomoko ya ardhi yaliyotokana na mvua kubwa mwishoni mwa wiki, imefikia 200, wakati shughuli za uokozi zikiimarishwa.

Ilielezwa kuwa vifo vingi vimeripotiwa katika mji mkuu wa Kathmandu ambao ulipata mvua nyingi zaidi na sehemu nyingi za kusini zilikumbwa na mafuriko.

Taarifa ya polisi ilisema kuwa watu 31 hawajulikani walipo, huku wengine 96 wakijeruhiwa.

Maporomoko ya ardhi pia yameripotiwa kuua idadi kubwa ya watu kwenye barabara iliyokuwa haipitiki kwa takriban kilomita 16 kutoka Kathmandu.

Ilielezwa kuwa maporomoko hayo yalifunika takriban mabasi matatu pamoja na magari mengine ambako watu walikuwa wamelala kwa kuwa barabara ilikuwa haipitiki.

Ilibainishwa kuwa barabara kuu tatu za kuingia Kathmandu zilizibwa na maporomoko ya ardhi kwa wikiendi nzima.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa hadi kufikia jana, wafanyakazi waliweza kufungua barabara kuu ya Prithvi, kwa kuondoa mawe, matope na miti ambayo ilikuwa imesombwa na maji kutoka milimani.

Ofisi ya Waziri Mkuu wa Nepal, Khadga Prasad Oli, ilisema baada ya kiongozi huyo kurejea nchini humo akitoka kushiriki mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa New York, Marekani aliitisha kikao cha dharura.

***VOA***



Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, akitoa onyo jana kwa Iran kwamba hakuna eneo lolote wasiloweza kulifikia huko Mashariki ya Kati. **PICHA: MTANDAO.**

# NATO yapata kiongozi mpya

**NATO**

JUMUIYA ya Kujihami ya NATO imepata kiongozi mpya Mark Rutte, ambaye ni Waziri Mkuu wa zamani wa Uholanzi anayechukua nafasi ya Jens Stoltenberg aliyehudumu kwa miaka 10.

Ilielezwa kuwa Julai 2023, Mark Rutte alitangaza kujiuzulu katika wadhifa wake wa Waziri Mkuu wa Uholanzi na miezi michache baadaye akaanza kudhihirisha nia yake ya kumrithi Katibu Mkuu wa NATO, Jens Stoltenberg, ambaye alitangaza kuachia wadhifa huo Septemba mwaka huu.

Pia ilielezwa kuwa kwa miezi kadhaa, Rutte aliendesha kampeni yake ndani ya muungano wa NATO, huku viongozi wengi wakiwa tayari wanamfahamu alipokuwa waziri mkuu wa Uholanzi kwa zaidi ya miaka 13 na kufanya kazi na mashirika mbalimbali ya kimataifa.

Mwanahistoria huyo ambaye ni mgombea aliyepigiwa pia upatu na Rais wa Marekani, Joe Biden na viongozi wengi wa Ulaya, anakabiliwa na changamoto katika uongozi wake ikiwa ni pamoja na vita nchini Ukraine.

Ilielezwa kuwa kuhusu hatua za baadaye za Russia na hali ya wasiwasi ya kisiasa nchini Marekani kutokana na kutofahamu kwa sasa ni nani atakayeshinda urais.

Wakati wa hotuba ya kuaga, kiongozi anayemaliza muda wake Jens Stoltenberg alizielezea baadhi ya changamoto zinazoikabilia NATO akisema tangu achukue wadhifa wa katibu mkuu ulimwengu unaowazunguka umebadilika.

"Tumeshuhudia Russia ikiichukua kinyume cha sheria rasi ya Crimea, kuimarika kwa kundi linalojiita Dola la Kiislamu IS, uvamizi kamili wa Russia nchini Ukraine, ushindani unaokua wa China, janga la Covid 19, mashambulizi zaidi ya mtandaoni na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwenye usalama wetu," alisema.

Mbali na hayo, Mark Rutte anakabiliwa pia na changamoto ya kuyaleta pamoja maono ya viongozi wa nchi wanachama ili kuwepo makubaliano ya pamoja kuhusu suala la maamuzi muhimu.

Ilielezwa kuwa Rutte ni mzoefu katika kuongoza miungano ya kisiasa nchini Uholanzi, lakini sasa atatakiwa kuvileta pamoja vyama 32 ili kufikia mwafaka unaohitajika kwa maamuzi yote ya NATO.

Katika kampeni yake, Rutte alikuwa na kibarua kigumu cha kumkinaisha Waziri Mkuu wa Hungary Viktor Orban, ambaye awali mahusiano yao yalikuwa na mkwaruzano.

Rutte alilazimika kumwahidi Orban kwamba Hungary haitalazimika kamwe kushiriki katika shughuli za kusaidia Ukraine nje ya eneo la NATO.

Ilielezwa kuwa siasa za kiliberali za Rutte na msimamo wa siasa kali za mrengo wa kulia za Orban mara nyingi huwaweka kwenye mzozo katika shughuli zao ndani ya Umoja wa Ulaya.

Uwezo wake mashuhuri wa kukabiliana na changamoto za kisiasa na kuwa na misimamo isioyumba, unamfanya Rutte kuwa kiongozi anayefaa iwapo Donald Trump atarejea katika Ikulu ya White House na kuanza ukosoaji wake dhidi ya muungano huo wa kijeshi.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Rutte ni muungwaji mkono mkubwa wa Ukraine na aliwezesha uwasilishaji wa silaha mjini Kyiv, ikiwa ni pamoja na vifaru na ndege za kivita chapa F-16.

***DW***

# Wabunge Kenya waonyesha kutokuwa na imani na Gachagua

**NAIROBI, Kenya**

WABUNGE nchini Kenya wanatazamiwa kuwasilisha hoja ya kumng'oa madarakani Makamu wa Rais, Rigathi Gachagua, katika bunge la taifa hilo.

Mbunge wa Kikuyu, Kimani Ichung'wah jana alithibitisha kuwa hoja dhidi ya Gachagua itawasilishwa mbele ya bunge na kujadiliwa.

Ilielezwa kuwa uwasilishaji wa hoja hiyo utahitaji kuungwa mkono na wabunge 233 na kuna taarifa zinazodai kuwa wajumbe 302 tayari wametia saini.

Pia ilielezwa kuwa wanaomshtaki Gachagua wanadai kuwa amekiuka Kifungu cha 10 cha katiba, wakisema matamshi yake hadharani yamekuwa ya uchochezi na yanaweza kuibua chuki za kikabila.

Aidha, ilielezwa kuwa anatuhumiwa kukiuka vifungu vya 147, 148,174,186 na 189 vinavyozungumzia mwenendo na wajibu wake kama msaidizi mkuu wa rais.

Ilielezwa kuwa atapewa nafasi ya kujitetea dhidi ya madai ya kujipatia mali kwa ufisadi na kutumia pesa za walipa kodi kwa njia isiyo halali. Na kwamba mali hiyo inasemekana kusambazwa katika kaunti za Nyeri, Nairobi na Kilifi.

Ikiwa hoja hiyo itakamilika, Spika wa Bunge la Taifa, Moses Wetangula atawasilisha azimio hilo kwa Spika wa Bunge la Seneti, Amason Kingi ndani ya siku mbili ili achukuliwe hatua.

Hoja ya kumwondoa madarakani Gachagua inakuja huku kukiwa na uhusiano wa mvutano baina ya Rais William Ruto.

Ilielezwa kuwa viongozi hao wawili wamekuwa wakitupiana lawama kila mmoja akidai mwenzake anakwamisha utendaji wa mwenzake.

***BBC***

**Aidha, ilielezwa kuwa anatuhumiwa kukiuka vifungu vya 147, 148,174,186 na 189 vinavyozungumzia mwenendo na wajibu wake kama msaidizi mkuu wa rais.**

# Wasanii 200 kushiriki tamasha la muziki Dar

Na Moshi Lusonzo

ZAIDI ya wasanii 200 kutoka mataifa mbalimbali watashiriki tamasha la kimataifa la muziki la ‚Marafiki-Haba na Haba' litakaloanza kesho katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Akizungumza na vyombo vya habari jana, Mkurugenzi wa Taasisi ya Asedeva, Isack Abeneko, amesema tamasha hilo litajumuisha muziki wa kizazi kipya, muziki wa asili, dansi, ngoma za asili na utoaji wa mafunzo mbalimbali ya sanaa hiyo.

Alisema matamasha ya ‚Marafiki-Haba na Haba' hapo awali yalikuwa yakifanyika katika miezi tofauti, lakini kwa mwaka huu wameamua kuyaunganisha ili kuwapa mashabiki wa muziki ladha ya kipekee katika burudani.

Abeneko, alieleza katika tamasha hilo kutakuwa na majukwaa mawili makubwa, moja likiwa katika viwanja vya Makumbusho, Dar es Salaam na lingine Bagamoyo.

Aliwataja baadhi ya wanamuziki maarufu wa Tanzania watakaotumbuiza kuwa ni Sholo Mwamba, Amini, Mabantu Band na Barobaro.

Aidha, wasanii wengine wanatoka katika nchi mbalimbali zikiwamo Cameroon, Rwanda, Kenya, Afrika Kusini, Angola, Togo, Nigeria na Ulaya.

"Kutakuwa na mafunzo ya muziki kwa wasanii wa hapa nchini ambayo yatatolewa na wanamuziki wakubwa barani Afrika, lengo letu ni kuufanya muziki kuwa sehemu ya maendeleo ya kiuchumi badala ya burudani pekee," alisema.

Aidha, aliishukuru serikali kupitia Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) kwa kusaidia kukamilisha maandalizi ya tamasha hilo ambalo ni sehemu ya jukwaa linalotambulisha utamaduni wa Tanzania.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni cha Ujerumani (Goethe), Mpangi Otte, alisema wameamua kusaidia tamasha hilo kutokana na ukweli kuwa muziki unawaweka watu pamoja bila kujali mipaka ya nchi.

Alisema nchi yake inatambua utamaduni ni sehemu ya kuhifadhi historia na utambulisho wa taifa husika, hivyo kuna umuhimu wa kuufanya uishi kupitia majukwaa ya muziki.

# SINGIDA BS YAFUATA POINTI TATU KIGOMA

Na Shufaa Lyimo, ARUSHA

KIKOSI cha Singida Black Stars jana kimeanza safari ya kuelekea Kigoma kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mashujaa huku wakiwa na matumaini ya kuondoka na pointi zote tatu.

Timu hizo zinatarajiwa kuumana Oktoba 4 kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema msafara umeondoka ukiwa na wachezaji 22 wanaofuata pointi hizo tatu.

"Kwa sasa tupo njiani tunaelekea Kigoma kwa ajili ya mchezo wetu ambao wa Oktoba 4, tumejiandaa vizuri na mpango wetu wa kwanza ni kuondoka na pointi zote tatu, tunaamini jambo hili linawezekana kutokana na maandalizi yetu," alisema Masanza.

Alisema kila mchezaji ana morali ya juu kuelekea kwenye mchezo wao huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa.

Alisema malengo yao msimu huu ni kuhakikisha wanashika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunataka kushiriki mashindano ya kimataifa, ili tupate hiyo nafasi ni lazima tuhakikishe tunapambana na kumaliza ligi kwenye nafasi za juu zaidi, tumejiwekea malengo ya kufanya hivyo," alisema Masanza.

Aidha, amewaomba mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano ili waendelee kuonyesha ushindani kwenye Ligi Kuu msimu huu.




Wachezaji wa SGA wakichuana katika mchezo wa mpira kwenye bonanza la maadhimisho ya miaka yake 40 lililofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# New City hali tete Ligi Kuu Zanzibar

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya New City FC imeendelea kupata matokeo mabaya mfululizo katika michezo mitatu waliyocheza ya Ligi Kuu ya Zanzibar.

New City FC juzi katika mchezo wao wa tatu dhidi ya Zimamoto SC walijikuta wakipoteza kwa kufungwa bao 1-0 mchezo uliochezwa Viwanja vya Amaan Nje saa kumi Alasiri.

New City FC ndio timu pekee ambayo haina alama katika msimamo wa ligi na inaburuza mkia kati ya timu 16 zinazocheza ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Razak Arajab alisema tatizo kubwa lililopelekea kushindwa kufanya vizuri ni kukosa maandalizi ya mapema.

Alisema kukosa maandalizi ya mapema yalitokana na ukata wa fedha ulioikumba timu hiyo hasa pale kuchelewa kupata fedha za udhamini wa ligi hiyo.

"Michezo miwili ya awali wachezaji walicheza tusema kishingo upande au kwa kuvunjika moyo kwa kuona kama hatuwapi pesa, lakini hivi sasa wamepewa fedha zao ndio maana mchezo wa leo walicheza vizuri licha ya kutopata matokeo mazuri," alisema.

Alisema timu yake imeanza kunyanyuka katika mchezo huo watatu kwa kucheza vizuri ikilinganishwa michezo miwili iliyopita licha ya kutopata alama tatu.

Alisema mchezo wao dhidi ya Zimamoto SC ulikuwa mgumu kutokana na timu zote hazikuwahi kupata matokeo ya ushindi tangu kuanza ligi.

"Mbali na maandalizi duni lakini mchezo huu ulikuwa wa vita ya matokeo, sisi tulihitaji na wao walihitaji lakini bahati iliangukia kwao," alisema.

Katika ligi hiyo bingwa mtetezi JKU SC wanaongoza kwenye msimamo kwa kufukisha alama tisa sawa na Muembe Makumbi City ambao wamezidiwa uwiano wa magoli ya kufunga na kufungwa, nafasi ya tatu inashikiliwa na Malindi SC yenye pointi saba.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### W' HAM YAMTAKA DURAN
CHELSEA na West Ham ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 20. ***(Give Me Sport)***

### N' FOREST KUMUUZA MURILLO
KLABU ya Nottingham Forest itamuuza Murillo bila kutaka, ikiwa watapokea ada kubwa kwa beki huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Barcelona na Real Madrid. ***(Football Insider)***

### JAMAL MUSIAL NA BAYERN
WINGA wa Ujerumani, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 21, ambaye mkataba wake na Bayern Munich utatamatika mwaka 2026, alisema alikuwa wazi kwa kila kitu lakini ana furaha sana kwamba huenda siku moja akacheza Ligi Kuu ya England. ***(Guardian)***

### ALEX BAENA AVUTIA EPL
WINGA wa Villarreal raia wa Hispania, Alex Baena mwenye umri wa miaka 23, amewavutia maskauti wa Aston Villa na Newcastle United msimu huu. ***(Caught Offside)***

### BAYERN WAJIVUNIA OLISE
WAKUU wa Bayern Munich wanaamini kuwa walimsajili nyota wa pauni milioni 100 kwa nusu bei pale walipoishinda Manchester United kwenye usajili wa pauni milioni 50 wa winga wa Ufaransa, Michael Olise mwenye umri wa miaka 22 kutoka Crystal Palace. ***(Mirror)***

### POTTER ATAJWA S'HAMPTON
KLABU ya Southampton inaweza kumgeukia kocha wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter iwapo wataamua kumfukuza, Russell Martin. ***(Football Insider)***

### EZE AMERIDHIKA C'PALACE
WINGA wa England, Eberechi Eze ameridhika na nafasi yake huko Crystal Palace, ambao walishangazwa kutopokea ofa kutoka kwa klabu za Ligi Kuu England wakati wa msimu wa huu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### WILSON KUONDOKA N'CASTLE
KLABU ya Newcastle United iko tayari kumruhusu mshambuliaji wa England, Callum Wilson mwenye umri wa miaka 32 kuondoka bila malipo msimu ujao iwapo hawatapata mbadala wake Januari. (Give me Sport)

### YAZICI KUSAINI OLYMPIAKOS
MSHAMBULIAJI wa Uturuki, Yusuf Yazici mwenye umri wa miaka 27 anatazamiwa kusaini mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Ugiriki ya Olympiakos baada ya kuondoka katika klabu ya Lille ya Ufaransa. ***(Fabrizio Romano)***

### REAL MADRID YAMTAKA PAZ
REAL Madrid inafuatilia hatua za Nico Paz huko Como na inaweza kukiamsha kipengele cha kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 20 ikiwa ataendelea kuonesha kiwango kizuri cha mchezo akiwa na timu hiyo ya Serie A. ***(AS)***

### DYCHE ATAKA KUBAKI EVERTON
SEAN Dyche ameelezea wazi nia yake ya kutaka kubaki kama kocha wa Everton baada ya klabu kununuliwa hiyo na kuwaongoza katika uwanja wao mpya. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MABOSI 'WAMKUMBATIA' TEN HAG MAN UNITED

**Licha ya vipigo vikubwa kutoka kwa Liverpool na Tottenham, bado wameendelea ...**

**MANCHESTER, England**

MABOSI wa klabu ya Manchester United bado wana nia ya kuendelea kumuunga mkono kocha Erik ten Hag licha ya kipigo kikubwa cha mabao 3-0 kutoka kwa Tottenham Hotspur, vyanzo vimeiambia ESPN.

Kwa mujibu wa chanzo hicho, kuna kukubalika kuwa Mholanzi huyo licha ya sasa kuwa chini ya shinikizo kubwa mbele yake kuelekea mechi muhimu dhidi ya FC Porto na Aston Villa wiki hii.

Vichapo vizito vya nyumbani kutoka kwa Liverpool na Spurs msimu huu tayari vimemweka kwenye presha kubwa.

Klabu hiyo iko tayari kuheshimu uamuzi wao walioutoa msimu wa majira ya joto wa kuendelea kuwa Ten Hag kwa sasa, lakini hisia bado ni kwamba lazima kuwe na uboreshaji mkubwa wakati timu hiyo itakabiliana na Porto kwenye Ligi ya Europa siku ya Alhamisi na Villa kwenye Ligi Kuu England Jumapili.

Mchezo huo utakaopigwa Villa Park ni wa mwisho kwa United kabla ya mapumziko ya wiki mbili ya kimataifa.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba vipigo vya nyumbani dhidi ya Liverpool na Spurs vimesababisha wasiwasi mkubwa klabuni hapo.

Namna ya uchezaji dhidi ya timu hizo mbili, pamoja na uchezaji duni katika kipindi cha pili cha sare ya 1-1 na FC Twente wiki iliyopita vinachukuliwa kuwa ni hali ya kutisha.

United wanaamini kuwa wamejiandaa vyema kufanya mabadiliko iwapo matokeo na aina ya uchezaji haubadiliki.

Msaidizi wa Ten Hag, Ruud van Nistelrooy angalau katika muda mfupi anachukuliwa kuwa chaguo linalowezekana ikiwa mabadiliko yatahitajika.

Van Nistelrooy ana uzoefu wa usimamizi na PSV Eindhoven na anaungwa mkono na msaidizi mwenzake, Rene Hake, ambaye alikuwa kocha mkuu wa FC Utrecht na Go Ahead Eagles ya Uholanzi kabla ya kujiunga na United.

Mabosi wa klabu akiwamo mmiliki mwenza Sir Jim Ratcliffe na Mkurugenzi wa michezo wa INEOS, Sir Dave Brailsford, walizungumza na makocha tofauti majira ya joto na kuna imani kwamba mchakato wa kuajiri utapunguzwa sana baada ya kufanya uangalizi wa kutosha kwa baadhi ya wasimamizi wanaotarajiwa katika mwisho wa msimu uliopita.

Chanzo kimoja kimeiambia ESPN kwamba klabu hiyo itazingatia hali hiyo kwa makini katika siku zijazo na inasitasita kuingia kwenye kuajiri kocha mpya.

Kurejesha kwa United pointi saba kutoka mechi sita za kwanza ndio mwanzo wao mbaya zaidi kuwahi kutokea kwenye kampeni za Ligi Kuu.

Pia wamepoteza mechi mfululizo za nyumbani kwenye ligi bila kufunga bao kwa mara ya kwanza tangu Novemba 2021 katika mechi mbili za mwisho za Ole Gunnar Solskjaer huko Old Trafford kabla ya kutimuliwa.

# GRIEZMANN ASTAAFU UFARANSA



**MADRID,** HISPANIA

ANTOINE Griezmann amestaafu kucheza soka la kimataifa baada ya miaka 10 akiwa na timu ya taifa ya Ufaransa, mchezaji huyo ametangaza.

Griezmann mwenye umri wa miaka 33, alikuwa sehemu muhimu ya timu za Ufaransa ambazo zilifika fainali tatu na kupoteza fainali ya Euro 2016 katika ardhi ya nyumbani, kushinda Kombe la Dunia 2018 na kuchapwa katika fainali ya Kombe la Dunia 2022 na pia kushinda Ligi ya Mataifa ya UEFA 2021.

Mechi za mwisho za mshambuliaji huyo wa Atlético Madrid akiwa na Ufaransa zilikuja katika michezo ya mwezi wa tisa, baada ya kuwa sehemu ya timu ambayo ilifungwa kwenye nusu fainali ya Euro 2024 na Hispania.

„Ni kwa moyo uliojaa kumbukumbu kwamba ninafunga sura hii ya maisha yangu," alisema Griezmann kupitia chapisho la kwenye mtandao wa kijamii.

„Asante kwa tukio hili zuri, lenye rangi tatu, na tutaonana hivi karibuni."

„Leo, kwa hisia kali, natangaza kustaafu kwangu kama mchezaji wa timu ya taifa ya Ufaransa," alisema Griezmann.

„Baada ya miaka kumi ya ajabu yenye changamoto, mafanikio na nyakati zisizosahaulika, ni wakati wa mimi kufungua ukurasa na kutoa nafasi kwa kizazi kipya.

„Kuvaa jezi hili imekuwa heshima na fursa ninaondoka kwenye timu ya taifa ya Ufaransa kwa hisia ya fahari na shukrani. Nilipata heshima ya kuiwakilisha nchi yetu, na fursa ya kupata matukio ya ajabu, kama vile kuwa bingwa wa dunia.

„Nitaendelea kuifuatilia Les Bleus kwa shauku. Nina hakika kwamba siku zijazo ni nzuri na siwezi kusubiri kuona kizazi kijacho kikiangaza."

Griezmann alicheza mechi yake ya kwanza ya Ufaransa Machi mwaka 2014, katika ushindi wa 2-0 wa kirafiki dhidi ya Uholanzi.

Kocha wake katika maisha yake yote ya kimataifa amekuwa Didier Deschamps, ambaye amekuwa akiinoa nchi yake tangu mwaka 2012.

Mwaka 2016, Griezmann alicheza mechi saba Ufaransa ilipotinga fainali ya Ubingwa wa Ulaya ambapo walichapwa 1-0 na Ureno.

Miaka miwili baadaye, alianza kila mchezo huku Ufaransa ikitwaa ubingwa wa Kombe la Dunia nchini Urusi, akifunga mabao manne, likiwamo penalti kwenye fainali dhidi ya Croatia.

Alipata sifa kwa kucheza katika nafasi ya kiungo aliyejiondoa zaidi wakati Ufaransa ilipotinga fainali ya Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, ambapo walifungwa kwa mikwaju ya penalti na Argentina.

Griezmann aliichezea Ufaransa jumla ya michezo 137, akifunga mabao 44. Alianza kwa Atlético katika sare ya 1-1 dhidi ya Real Madrid kwenye LaLiga Jumapili.

Mshambulizi huyo mara kwa mara amesema angependa kumalizia soka lake nchini Marekani.

## Foden atarajiwa kurejesha ubora wake

**MANCHESTER,** ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Phil Foden, amekuwa na shida kufikia sasa kuongeza kiwango chake cha juu cha msimu uliopita, lakini Kocha Pep Guardiola amesema kampeni yake inakaribia kuimarika.

Foden alifunga mabao 28 kwa klabu na nchi katika michuano yote na alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Mwaka wa PFA, lakini ameanza mechi zake nne kati ya tano.

Akizungumza kabla ya mechi ya Ligi ya Klabu Bingwa Ulaya ugenini nchini Slovakia dhidi ya Slovan Bratislava, Guardiola alisema hana wasiwasi, akisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 anarejea kwenye kasi yake.

"Labda naweza kuwa na mashaka katika mambo mengi, lakini Phil Foden atarejea! Kadiri anavyojisikia vizuri, atarejea," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Nadhani katika dakika 30 pale St James' Park katika sare ya 1-1 dhidi ya Newcastle United Jumamosi, nilihisi tayari kitu ambacho nakipenda ambacho sikukiona kwa mfano dhidi ya Watford.

„Usisahau baada ya Euro hakuwa na mazoezi yoyote kwa miezi miwili, alikuwa na shida kadhaa za kiafya," alisema Guardiola. „Lakini sasa anatabasamu na yuko katika mdundo wake.

"Alikuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu msimu uliopita kwa hivyo tunamhitaji, alikuwa muhimu kwetu, lakini sina shaka na mapenzi yake kwa soka na mafunzo yake, atarejea."

City walitoka suluhu katika mchezo wao wa kwanza wa kundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa nyumbani dhidi ya Inter Milan.

## Flick: Hakuna uhakika wa namba moja kwa Szczesny



**BARCELONA,** HISPANIA

HANSI Flick amethibitisha kuwa tayari amezungumza na Wojciech Szczesny baada ya mlinda mlango huyo wa zamani wa Arsenal na Juventus kuwasili Barcelona siku ya Jumatatu kukamilisha uhamisho wake wa kujiunga na vinara hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Szczesny mwenye umri wa miaka 34, amekubali kutoka kustaafu na kuchukua nafasi ya Marc-André ter Stegen, ambaye ameondolewa kwa msimu huu kutokana na jeraha la goti, na sasa atawania namba na na Iñaki Peña.

Flick aliacha kuthibitisha usajili huo, lakini akasisitiza kuwa mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Poland hajapewa ahadi zozote kuhusu muda wa kucheza kwenye Uwanja wa Olimpiki.

"Kwa kawaida huwa sizungumzii kuhusu wachezaji ambao si sehemu ya kikosi, lakini naweza kusema kwamba hakuna mchezaji wa Barca aliye na hakikisho kwamba ataanza," alisema Flick alipoulizwa kama Szczesny aliahidiwa namba moja.

"Ndiyo, nimezungumza naye, lakini sitasema lolote zaidi ya hilo. Ikiwa katika siku zijazo atasaini Barca, tunaweza kuzungumza zaidi kuhusu hilo katika mkutano ujao wa waandishi wa habari.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba, Szczesny atasaini mkataba hadi mwisho wa msimu.

HABARI MICHEZO

# AHOUA AWABURUZA FEITOTO, AZIZ KI KWA 'ASSIST' LIGI KUU

**Na Mwandishi Wetu**

UKIWA ni msimu wake wa kwanza tu tangu ajiunge na klabu ya Simba, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Jean Charles Ahoua, ameonekana kuanza kuwa tishio kwa wachezaji wa Ligi Kuu kwa kutoa pasi za mwisho za mabao akiwa amefanya hivyo mara nne katika michezo minne aliyocheza.

Mpaka kufikia raundi ya sita, Ahoua anaonekana kuanza kuwaburuza wachezaji ambao ni wazoefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, na ambao walifanya vyema msimu uliopita kwenye ‚asisti', kama Feisal Salum wa Azam, Stephane Aziz Ki wa Yanga, Clatous Chama ambaye alikuwa Simba na sasa yupo Yanga, pamoja Mohamed Hussein wa Simba.

Ahoua, raia wa Ivory Coast aliyesajiliwa kutoka Stella Club d'Adjamé ya nchini humo, amecheza kwa dakika 289 katika michezo minne, akipachika mabao mawili na ‚asisti' nne, ambazo alizitoa katika michezo mitatu ambayo Simba ilicheza dhidi ya Fountain Gate, Agosti 25, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Simba ikishinda mabao 4-0 ambapo alitoa pasi za mabao kwa Edwin Balua na Valentino Mashaka, huku mwenyewe akipachika bao moja.

Kabla ya hapo, alifanya hivyo kwa Che Fondoh Malone, Agosti 18, Simba ikicheza dhidi ya Tabora United ikishinda mabao 3-0 kwenye uwanja huo huo.

Septemba 26, Uwanja wa New Amaan, Zanzibar, alitoa ‚asisti' kwa Leonel Ateba, Simba ilipocheza dhidi ya Azam FC na kushinda mabao 2-0.

Ikumbukwe msimu uliopita, Aziz Ki na Kipre Junior walikuwa vinara wa ‚asisti' wakiwa wamefanya hivyo mara nane.

Hata hivyo, raia huyo wa Ivory Coast anafuatiwa kwa karibu na Fei Toto, ambaye ana ‚asisti' tatu alizowapa Lusajo Mwaikenda na Idd Nado katika mchezo dhidi ya KMC, wakipata ushindi wa mabao 4-0, na Nassor Saadun katika mchezo dhidi ya Coastal Union, Azam ikishinda bao 1-0.

Aziz Ki, ana ‚asisti' mbili mpaka sasa, akitoa kwa Clement Mzize katika mchezo dhidi ya Kagera Sugar, Yanga ikishinda mabao 2-0 na dhidi ya Ibrahim Hamad ‚Bacca' katika mchezo dhidi ya KenGold Yanga wakishinda bao 1-0.

Wengine wenye ‚asisti' mbili ni Mohamed Hussein ‚Tshabalala', wa Simba, Ande Kofi wa Singida Black Stars, Salum Kihimbwa wa Fountain Gate, na Joseph Mahundi wa Kagera Sugar.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Lumumba (wenye jezi nyeupe), na wanafunzi wa Shule ya Msingi Yuniti ya Ukonga jijini Dar es Salaam, wakicheza mpira wa magongo juzi katika mashindano ya shule za msingi na sekondari yanayofanyika kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga yaanzisha operesheni kurejea kileleni Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema imeanza mkakati kabambe wa kuhakikisha inakwenda kukamata nafasi ya kwanza kwenye Ligi Kuu kuanzia kesho itakapocheza dhidi ya Pamba Jiji, Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema kuwa pamoja na kushinda michezo yao mitatu, lakini bado hawatokuwa na furaha hadi hapo watakapohakikisha wamekamata nafasi ya kwanza ambayo ndiyo sehemu waliyoizoea.

„Operesheni hii ni kuisaka namba moja, tutaianza rasmi Alhamisi tutakapocheza dhidi ya Pamba Jiji, niseme tu kuwa tuko katika harakati ya kuisaka nafasi ya kukaa kileleni, tumekusanya pointi tisa, tuko vizuri kidogo katika msimamo wa Ligi Kuu, ila nafasi yetu pendwa ni namba moja, tutaanza rasmi kuisaka kwenye mchezo dhidi ya Pamba Jiji, tunaelekea kileleni na hakuna wa kutuzuia," alisema Kamwe.

Hata hivyo, Kamwe amewaambia mashabiki wa timu hiyo kuwa jambo hilo halitokuwa rahisi kama wao watakaa majumbani, inabidi wajazane uwanjani kwa ajili ya kuwaunga mkono viongozi, benchi la ufundi pamoja na wachezaji kwani nguvu ya pamoja inatakiwa.

"Timu ambazo hazijaanza vyema zikicheza na Yanga zinakamia sana, tuliona mchezo na KenGold, tukashuhudia dhidi ya KMC, kwa hiyo hata Pamba Jiji haitokuwa rahisi, kwa hiyo mashabiki wanatakiwa wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kuungana katika mkakati wa kuelekea kwenye nafasi ya kwanza," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Habari wa Pamba Jiji, Moses William, akizungumza na gazeti hili alisema wamejiandaa kuwapa Yanga wakati mgumu katika mchezo huo.

Aidha, alikiri kuwa bado hawapo katika wakati mzuri, lakini haiwazuii kufanya vyema katika mchezo huo.

"Tunafahamu tunakwenda kucheza mchezo mgumu dhidi ya Yanga, ni timu bora na wameanza vizuri, sisi tumeanza vibaya ingawa haimaanishi kuwa tuna timu mbaya, matokeo hayajawa mazuri upande wetu, walimu watakuwa wameona mapungufu na watayarekebisha kuelekea katika mchezo huo," alisema Ofisa Habari huyo.

Alisema katika mechi hiyo watakwenda kwa tahadhari kubwa na kuwapa heshima wapinzani wao.

Wakati Yanga ikicheza michezo mitatu na kushinda yote ikiwa na pointi tisa na kushika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Pamba Jiji haijashinda mchezo wowote katika mechi sita ilizocheza, imetoka sare mechi nne na kupoteza miwili, inashika nafasi ya 14 kwa kukusanya pointi mbili.

## Kamati yawakingia kifua waamuzi

INATOKA UK. 24

Aliongezea kuwa kamati hiyo bado inaendelea kuwasisitiza waamuzi waendelee kuchezesha soka kwa kufuata sheria 17 kama wanavyofanya sasa.

Hivi karibuni kuliibuka malalamiko ya mashabiki baada ya mchezo kati ya Simba dhidi ya Dodoma Jiji ambapo baadhi walilalamikia adhabu ya penalti iliyotolewa kwa Simba na kuwapatia bao pekee kwenye mchezo huo.

Pia kulikuwa na malalamiko kwenye mchezo kati ya Yanga dhidi ya KenGold ambapo mwamuzi alilalamikiwa kwa kuwanyima goli KenGold.

## Samatta, Kibu warejeshwa Taifa Stars

INATOKA UK. 24

"Hakuna kitu kikubwa sana tulichowaitia hapa, ila ni kuwatajia kikosi kitakachocheza dhidi ya Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo.

Tutakuwa na wachezaji 23 ambao wataingia kambini Oktoba 4, na tutaondoka Oktoba 7 kwa ajili ya mchezo wa kwanza utakaochezwa Oktoba 10 na mechi ya marudiano itachezwa tarehe 15," alisema Morocco.

Mbali na Samatta anayeichezea PAOK FC Ugiriki, Kibu, Hamza wa Simba, na Mwalimu wa Fountain Gate, wengine walioitwa kwenye kikosi hicho ni, Ali Salim (Simba), Zuberi Foba na Yona Amos wa Pamba kwa upande wa makipa, wengine ambao majina ya klabu zao yako kwenye mabano ni mabeki ni Mohamed Hussein ‚Tshabalala' (Simba), Lusajo Mwaikenda na Paschal Msindo (Azam), Ibrahim Bacca, Bakari Mwamnyeto, Dickson Job (Yanga), Haji Mnoga (Salford City) ya England.

Viungo ni Feisal Salum, Adolf Mutasingwa (Azam), Habib Khalid (Singida Black Stars), Himid Mao (Talaal El Geish) ya Misri, Mudathir Yahaya (Yanga) na Cyprian Kachwele (Vancouver Whitecaps) ya Canada.

Washambuliaji ni Clemet Mzize (Yanga), Nassor Saadun (Azam) akichaguliwa kwa mara ya kwanza na Abdullah Saud wa KMC.

Kikosi hicho kinatarajia kuingia kambini Ijumaa kujiandaa na mchezo wa Oktoba 10 utakaochezwa uwanja wa Stade des Martyrs, jijini Kinshasa, kabla ya marudiano, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Oktoba 15.

Michezo
Jumatano Oktoba 2, 2024
Nipashe

**Mabosi 'wamkumbatia' Ten Hag Man United**

UKURASA 21



# KAMATI YAWAKINGIA KIFUA WAAMUZI L/KUU

● ● ● Yasema mpaka sasa hakuna makosa wala malalamiko yaliyofikishwa kwao, adhabu ni...

**Na Faustine Feliciane**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Nassoro Hamduni, amesema licha ya hivi karibuni kuibuka malalamiko juu ya waamuzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini kamati hiyo inaridhishwa kwa namna waamuzi hao wanavyofuata sheria zote za soka na adhabu wanazozitoa.

Baada ya mzunguko wa tatu wa Ligi Kuu, kumeibuka malalamiko kutoka kwa baadhi ya wadau wa soka juu ya maamuzi yanayotolewa na marefarii kwenye baadhi ya mechi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Hamduni alisema kimsingi kamati yake haijapokea malalamiko yoyote licha ya kukiri kusikia kwa mashabiki.

"Hatujapata malalamiko yoyote rasmi, kama kamati tunaona kila kitu kinaenda vizuri, mwamuzi ni mwanamichezo na anaendeshwa na kanuni za ligi, anapokosea anaadhibiwa na kamati ya waamuzi adharani na watu wanajua," alisema Hamduni.

Alisema kwa sasa yanayosikika ni malalamiko tu ambayo hawawezi kuyazuia ila Kamati inaridishwa na mambo yanavyoenda sawa mpaka sasa kufikia raundi sita zilizochezwa.

"Nawapongeza sana waamuzi kwa sababu wamechezesha vizuri na wanatoa adhabu pale inapostahili kulingana na kosa husika na kanuni zake," alisema.

INAENDELEA UK. 23



Samata

## Samatta, Kibu warejeshwa Taifa Stars

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Mbwana Samatta, amerejeshwa kwenye kikosi hicho, akiwa mmoja wa wachezaji 23 walioteuliwa kwa ajili ya kucheza michezo miwili ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazochezwa mwakani nchini Morocco.

Kocha wa Stars, Hemed Moroco, ameita wachezaji hao 23 kwa ajili ya michezo dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo itakayochezwa Oktoba 10 na 15.

Samatta hakuwamo katika michezo miwili ya Kundi H, ambayo Stars ilikipiga dhidi ya Ethiopia na Guinea, ambapo taarifa zilisema Samatta mwenyewe aliomba kumpumzika.

Hata hivyo, pamoja na matokeo ya suluhu dhidi ya Ethiopia na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Guinea, bado baadhi ya mashabiki walidai straika huyo bado anahitajika kwenye kikosi kwa jinsi walivyoona timu ikicheza kwenye michezo hiyo miwili.

Moroco, pia amemrudisha winga wa Simba, Kibu Denis ambaye naye hakuwamo katika michezo miwili iliyopita.

Beki mpya wa Simba, Abdurazack Hamza, na kinara wa mabao wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, Selemani Mwalimu wa Fountain Gate ni baadhi ya wachezaji walioitwa kwenye kikosi hicho.

Kocha huyo safari hii hakumjumuisha winga wa Simba, Edwin Balua, golikipa wa Yanga, Abdultwarib Mshery wala Waziri Junior wa Dodoma Jiji ambao walikuwapo kwenye kikosi kilichopita.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >